# SHERIA YA KUWEKA MASHARTI BORA YA USIMAMIZI WA USHURU WA STEMPU NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO NA KUFUTA SHERIA YA USHURU WA STEMPU NAM. 6 YA MWAKA 1996.

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**VIFUNGU VYA UTANGULIZI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Ufafanuzi.

**SEHEMU YA PILI**
**UTOZAJI KODI NA UTAWALA**

3. Utozaji kodi.
4. Hati ya kutokuwa na pingamizi.
5. Utawala

**SEHEMU YA TATU**
**MASHARTI YA JUMLA YANAYOHUSIKA NA HATI**

6. Hati zinazostahiki kutozwa kodi.
7. Watu anayewajibika kulipa.
8. Utambuzi.
9. Namna hati zitakavyoandikwa na kuwekwa stempu.
10. Adhabu kuhusiana na stempu ya kubandikwa.
11. Uwekaji wa stempu kwa baadhi ya hati.
12. Uchunguzi na uzuiaji wa hati.

13. Ufutwaji wa stempu.

14. Ufutaji kwa mawakala walioteuliwa.

15. Thamani ya mali inayostahiki kulipiwa kodi.

16. Maelekezo kuhusiana na ushuru wa baadhi ya hati za uhaulishaji mali.

17. Sehemu au upande.

18. Hati za uingizaji na usafirishaji wa bidhaa.

19. Hati ya malipo na hawala.

20. Uhaulishaji kwa njia ya mauzo.

21. Thamani ya malipo kwa vipindi.

22. Athari ya maelezo ya thamani.

23. Namna ya kuhesabu kiwango cha ushuru kwa asilimia.

24. Uhaulishaji wa makubaliano ya deni au malipo ya baadae kutozwa ushuru.

25. Rehani.

26. Uhaulishaji wa hiari.

27. Namna itakavyotozwa dhamana kwa malipo ya baadae.

28. Namna ya ukodishaji kutozwa mrahaba.

29. Ushuru wa ukodishaji kwa mazingira mengineyo.

30. Namna ya kutozwa ukodishaji katika uzalishaji au vyenginevyo.

31. Ushuru katika ukodishaji wenye kodi tofauti.

32. Hati hazitathibitishwa kwa kiapo mpaka ziwekwe stempu.

33. Sera za Bima.

34. Sera ya Bima ya usafiri wa bahari.

35. Mkataba wa ukodishaji chombo cha usafiri.

36. Kuwekwa stempu makubaliano ya ukodishaji kwa madhumuni ya kununua.

37. Utiaji thamani hisa na dhamana za soko.

38. Uhaulishaji wa nyaraka za hisa.

39. Uhaulishaji kwa njia za mauzo.

40. Fedha zinazostahiki kulipwa.

41. Ikiwa hati mbalimbali moja tu itatozwa.

42. Dhamana za hisa.

43. Hundi zilizokuwa hazijawekwa stempu.

44. Mfanyakazi wa benki au hawala ya benki.

45. Masharti ya kutozwa ushuru wa risiti.

46. Utaratibu wa ushuru katika risiti.

47. Ritani na malipo.

48. Hati zitakazotozwa ushuru tofauti.

49. Kivuli au nakala.

50. Hati ambazo hazijawekwa stempu hazitotumika kama ushahidi.

51. Kamishna kutoa maoni.

52. Uwezo wa Kamishna kurejesha malipo ya adhabu au ushuru uliozidi kwa baadhi ya mazingira.

53. Tathmini ya ushuru kwa mazingira maalum.

54. Muda wa kuweka stempu nyaraka.

55. Ruhusa kwa stempu zilizoharibika.

56. Mazingira ya stempu zilizoharibika.

57. Ruhusa katika kubadilisha stempu.

58. Thamani ya mtathmini wa Serikali.

59. Kumbukumbu za kielektroniki.

## SEHEMU YA NNE
## USHURU WA STEMPU KATIKA UENDESHAJI WA BIASHARA

60. Viwango vya kutozwa.

61. Shughuli inayotozwa kodi.

62. Thamani inayotozwa kodi.

63. Utambulisho wa walipa kodi.

64. Udhibiti, tathmini na ukusanyaji.

65. Kutambuliwa malipo ya ushuru wa stempu.

66. Ritani na maelezo yake.

67. Ukadiriaji wa thamani.

## SEHEMU YA TANO
## MENGINEYO

68. Kushindwa kuonesha maelezo sahihi kuhusiana na hati.

69. Usajili wa hati zisizowekewa stempu sahihi.

70. Kuweka kikwazo katika usimamizi wa Sheria hii.

71. Makosa yanayohusiana na kuweka stempu katika hati, kuharibu na ukwepaji ushuru.

72. Kumiliki hati ambazo zimewekwa stempu kinyume na Sheria.

73. Stempu zilizoghushiwa.

74. Adhabu za jumla.

75. Uwezo wa kuchunguza.

76. Uwezo wa kupata taarifa.

77. Uwezo wa kusamehe malipo ya ushuru katika hati.

78. Kanuni.

79. Kufuta na kubakiza.

**SHERIA NAMBA 7 YA 2017**

**NIMESAINI**

**{DR. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

27 Julai, 2017

# SHERIA YA KUWEKA MASHARTI BORA YA USIMAMIZI WA USHURU WA STEMPU NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO NA KUFUTA SHERIA YA USHURU WA STEMPU NAM. 6 YA MWAKA 1996.

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## VIFUNGU VYA UTANGULIZI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Ushuru wa Stempu ya mwaka 2017 na itaanza kutumika mara baada ya kusainiwa na Rais.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"afisa aliyeidhinishwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeidhinishwa chini ya masharti ya Sheria hii na Kamishna au mamlaka nyengine yoyote iliyopewa uwezo kufanya hivyo, kutekeleza kazi yoyote kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

"afisa wa Umma" inajumuisha afisa yeyote aliyeteuliwa na Serikali kutekeleza majukumu ya Umma aliyopewa kwa mujibu wa Sheria au maelekezo na inajumuisha pia msuluhishi au mtu mwengine yeyote ambaye kisheria au kwa idhini ya pande zinazohusika ana uwezo wa kupokea ushahidi;

"Uthibitisho" maana yake ni barua ya uthibitisho ambayo inathibitisha deni lolote au dai au sehemu yake yoyote kuwa limefanyika, limelipwa au limekuwa la kuridhisha kama itakavyokuwa;

"kilichoambatanishwa" kuhusiana na stempu ya kubandika maana yake iliyoambatanishwa kwa umakini kwa kutumia gundi la kuwekea stempu;

"kiwango kinachokubalika" maana yake ni msingi unaokubalika na kupendelewa Kimataifa kwa kuainisha thamani ya uhaulishaji wa muamala baina ya watu wenye mahusiano;

"Muombaji" maana yake ni mtu aliyeomba kufanya makubaliano chini ya Sheria hii na inajumuisha Wawakilishi binafsi walioidhinishwa na mawakili wake;

"kushuhudiwa" maana yake ni kushuhudiwa kwa kutiwa saini na Mamlaka yenye uwezo kwa namna iliyoelezwa katika kuonesha malipo halali ya ushuru wa stempu;

"mfanyakazi wa benki" na "benki" inajumuisha Shirika, Jumuiya, Ushirika au mtu anayefanyakazi za kibenki Zanzibar;

"Hati ya malipo" inajumuisha hawala, agizo la malipo, hundi,hati ya uthibitisho wa malipo na hati nyengine yoyote inayohusu au inayotoa ruhusa kwa mtu mwingine ama ametajwa au hakutajwa ndani ya hati hiyo kwa malipo ya mtu mwingine au kupokea kwa niaba ya mtu mwingine kiwango chochote cha fedha;

"Hati ya usafirishaji wa mizigo" inajumuisha risiti yoyote iliyotolewa kutoka kwa mkuu wa chombo, mwenza, mmiliki au wakala wa chombo chochote na haikuwekwa stempu baada ya kutolewa;

"biashara" inajumuisha shughuli yoyote inayofanywa kwa lengo la kujipatia faida au pato na pia inajumuisha biashara, uchumi au utengenezaji wa bidhaa;

"hati ya kutokuwa na pingamizi" maana yake ni hati iliyotolewa na Kamishna chini ya Sheria hii kuthibitisha thamani ya mali yoyote inayokusudiwa kuuzwa;

"Kinachopaswa kutozwa" maana yake ni kinachotozwa Ushuru wa Stempu chini ya Sheria hii au kinachotozwa chini ya sheria nyengine yoyote inayotumika Zanzibar kwa wakati husika kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii;

"viwango vinavyotozwa" maana yake ni viwango vilivyowekwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria hii;

"mkataba wa ukodishaji chombo" inajumuisha makubaliano au mkataba wowote wa ukodishaji chombo chochote cha usafiri baharini au angani au makubaliano yoyote,

barua, au maandishi mengine baina ya nahodha, mkuu wa chombo, mmiliki au wakala wa chombo chochote cha usafiri wa baharini na mtu mwengine yoyote, au inayohusiana na usafirishaji au uhaulishaji nje ya Zanzibar kwa fedha yoyote, biadhaa au vitu vilivyomo ndani ya chombo hicho;

"Hundi" maana yake ni hati ya malipo inayotolewa kwa utaratibu wa kibenki ulioainishwa na inayolipwa kwa mahitaji na sio vyenginevyo;

"Kamishna" maana yake ni Kamishna wa Bodi ya Mapato Zanzibar au mtu yoyote aliyemkasimia jukumu lolote katika majukumu yake chini ya Sheria hii;

"Hati ya kuhaulisha mali" inajumuisha hati ya mauzo na kila hati ambayo kutokana na hiyo mali inayohamishika au isiyohamishika imehamishwa kwa hiari kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine na ambayo haikutajwa katika jadweli chini ya Sheria hii na vile vile Sheria au amri inayohusiana nayo au yenye nguvu ya kuzuia;

"Mamlaka yenye uwezo" maana yake ni afisa aliyeteuliwa na Serikali kutekeleza majukumu ya Mamlaka yenye uwezo chini ya Sheria hii kwa jina lolote itakayoitwa.

"Kampuni " inajumuisha kampuni yoyote iliyoanzishwa Zanzibar au ikiwa imeanzishwa nje ya Zanzibar iliyosajiliwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar;

"Mahkama" maana yake ni Mahkama ya kisheria yenye uwezo katika eneo ambalo mlipa kodi au mtu anayehusika kawaida anaishi au anaendesha biashara yake au taaluma;

"Mlipa kodi aliyeshindwa" maana yake ni mlipa kodi ambaye ameshindwa kulipa ushuru wa stempu inayotozwa chini ya Sheria hii ndani ya kipindi kilichowekwa na kwa namna ilivyoelezwa;

"Mamlaka ya Rufaa iliyowekwa" maana yake ni mamlaka ya rufaa ya kodi ilivyoanzishwa na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi;

"Kuwekwa Stempu sahihi" maana yake ni hati iliyowekwa stempu ya kubandikwa au ya kugongwa isiyopungua kiwango sahihi kinachokubalika na kwamba stempu hiyo imefutwa na kushuhudiwa katika utaratibu uliowekwa;

"Ushuru" maana yake ni ushuru wowote unaotozwa kwa njia ya stempu chini ya Sheria hii au sheria nyengine;

"tarehe ya kupokea" maana yake, katika kupokea mali kwa njia ya muamala, tarehe ambayo muamala huo umefanywa, bila kujali kuwa muamala huo ulikuwa wa masharti au bila ya masharti au umefanywa kwa maslahi ya kampuni ambayo tayari imesajiliwa au kwa niaba ya kampuni itakayosajiliwa na, katika kupokea mali isiyokuwa kwa utaratibu wa miamala, tarehe ambayo kwa mtu ambae amepokea mali hiyo itakuwa na haki ya kuidai;

"Kukamilishwa" na Kamilika" inapotumika katika hati maana yake ni kutiwa saini na muhuri;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na inajumuisha mashirika yake;

"Muingizaji" maana yake ni muingizaji wa bidhaa zilizosamehewa kulipiwa kodi chini ya Sheria hii;

"Hati" inajumuisha waraka ambao unatoa haki au jukumu lolote au unatoa haki au jukumu, kuhaulisha, kuweka mipaka, kuongeza muda, kumalizika au kusajiliwa;

"sera ya muda ya bima" maana yake ni hati yoyote iliyotolewa Zanzibar ambayo inakusudiwa kukabili hatari yoyote chini ya mkataba wa bima unaosubiri kupatiwa risiti nje ya Zanzibar ya sera kamili ya kukabili hatari kama hiyo;

"Kukodisha" maana yake ni kukodisha mali isiyohamishika na inajumuisha:

(a) hati ya umilikaji;

(b) ruhusa ya kutumia na kunufaika na haki za asili au faida au haki ya kutumia kitu bila ya kupewa idhini rasmi;

(c) Hati yoyote ambayo tozo la aina yoyote limeruhusiwa;

(d) maandishi yoyote ya maombi ya kukodisha yanayokusudia kuonesha kuwa ombi limekubaliwa;

"Vifaa" inajumuisha kifaa chochote ambacho maneno au alama vinaweza kuelezewa;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na masuala ya fedha;

"Hati ya Rehani" inajumuisha hati yoyote ambayo kwa madhumuni ya usalama wa fedha iliyotolewa au itakayotolewa kwa njia ya mkopo au deni liliopo au la baadae au utekelezaji wa makubaliano mtu anatoa au anahamishia kwa maslahi ya mwingine haki juu ya mali yake iliyoainishwa na kwa madhumuni ya Sheria hii inajumuisha gharama chini ya sheria zinayohusiana na usajili wa ardhi;

"Hati ya uwakala" inajumuisha hati yoyote inayompa uwezo mtu maalumu kutekeleza chochote kwa niaba na kwa jina la mtu aliyeitia saini;

"hawala" inajumuisha hati yoyote inayothibitisha malipo ya kima chochote cha fedha kutoka katika mfuko maalum unaoweza au usiyoweza kupatikana au kwa masharti yoyote au dharura inayoweza au isiyoweza kutekelezwa au kutokea.

"jumla ya marejesho ya fedha kwa vipindi" maana yake ni jumla ya fedha iliyopokelewa au iliyolipwa na mlipa kodi kutokana na mauzo ya bidhaa au huduma katika kipindi maalum kilichoainishwa chini ya masharti ya Sheria hii;

"pahala pa biashara au taaluma" inajumuisha jengo au nyumba yoyote ambayo shughuli yoyote inayohusiana na biashara au taaluma, vyovyote itakavyokuwa, inafanyika hii inajumuisha uwekaji wa vitabu vya hesabu ya fedha, nyaraka na kumbukumbu;

"sera ya bima" inajumuisha maandishi yoyote ambayo mkataba wa bima umefanywa, umetolewa, umekubaliwa kufanywa, ambao unakusudiwa kuhakikishia usalama wa mali au huduma ndani ya mkataba wa bima Zanzibar;

"sera ya bima ya maisha" maana yake ni sera ambayo maisha au tukio lolote au dharura inayohusiana na au inayotegemea maisha, isipokuwa sera ya bima dhidi ya ajali kwa mtu au kuhusiana na kuumia, kutokuwa na uwezo wa kufanya kazi, ugonjwa au kinachofanana na hayo, au sera ambayo kiwango cha fedha kinachostahiki kulipwa fidia au hasara iliyopo chini ya Sheria yoyote inayohusiana na fidia kwa wafanyakazi au wajibu wa waajiri au chini ya Sheria ya nchi za Jumuiya za madola, kuhusiana na kifo au ugonjwa au kuumia kwa muajiriwa;

"Taaluma" inajumuisha kazi yeyote inayofanywa kwa madhumuni ya kujipatia maisha au kipato;

"mali" maana yake ni mali isiyohamishika au inayohamishika ya aina yoyote na inajumuisha haki yoyote inayoambatana na mali hiyo;

"risiti" au "hati ya mauzo" kutokana na mahusiano ya kibiashara au taaluma inajumuisha, barua, hati, au maandishi yoyote ambayo fedha zozote, hati ya malipo ya fedha, hundi au hawala yoyote imekubaliwa kuwa imepokewa au bidhaa au huduma yoyote itaelezwa kuwa imetolewa kwa mkopo kama itakavyokuwa;

"robo mwaka" maana yake ni kipindi baina ya tarehe 1 Januari hadi 31 Machi au tarehe 1 Aprili hadi 30 Juni au tarehe 1 Julai hadi 30 Septemba au tarehe 1 Oktoba hadi 31 Disemba ya mwaka wa fedha au mwaka wa kalenda;

"mauzo" inajumuisha mabadilishano na mfumo mwengine wowote wa kuhaulisha bidhaa na huduma kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mtu mwengine kwa malipo.

"kiwango maalumu" maana yake ni kiwango kilichoainishwa chini ya Sheria hii ambacho mlipa kodi hatawajibika kulipa kodi ya ongezeko la thamani;

"iliyowekwa stempu" kuhusiana na hati au vifaa maana yake ni hati au vifaa ambavyo kugongwa stempu kwa thamani halisi kwa njia ya stempu ya alama kwa thamani halisi au kwa stempu ya wazi kwa thamani halisi;

"ushuru wa stempu" inajumuisha malipo yoyote yanayolipwa kwa njia ya kodi, adhabu, faini, au kima chengine chochote kinachotozwa chini ya Sheria hii;

"mtu" inajumuisha mtu anayepaswa kulipa ushuru wa stempu au anayehusika kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii na inamjumuisha muwakilishi wake, aliowaidhinisha na wanaofanya kazi kwa niaba yake;

"maslahi ya umma" maana yake ni maslahi ya ustawi wa jumla wa umma ambayo yanahitaji kutambulika na kulindwa;

"kinachostahiki kulipiwa kodi" maana yake ni bidhaa au huduma zinazotozwa kodi chini ya Sheria hii;

"kutowekwa stempu" maana yake ni kutokuwekwa stempu ipasavyo kama inavyotakiwa na Sheria hii au sheria nyengine yoyote;

"kuandika", "kilichoandikwa", "kinachoandikwa" inajumuisha utaratibu wowote ambao maneno au kiwango kinaweza kuekwa kwenye kifaa;

## SEHEMU YA PILI
## UTOZAJI KODI NA UTAWALA

Utozaji kodi

**3.**-(1) Kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, kutatozwa na kukusanywa kodi itakayojulikana kama Ushuru wa stempu.

(2) Ushuru wa stempu chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki utatozwa na kukusanywa:

(a) katika usambazaji wa bidhaa na huduma Zanzibar na mlipa kodi kutokana na au uendeshaji wa biashara unaofanywa na mlipa kodi huyo;

(b) katika usambazaji wa bidhaa na huduma zilizosamehewa kulipa kodi chini ya Jadweli la Pili la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Nam. 4 ya mwaka 1998;

(c) kwa hati zote zilizoainishwa chini ya Jadweli la Kwanza la Sheria hii isipokuwa kwa hati zilizoainishwa kuwa zimesamehewa kulipiwa ushuru au;

(d) kwa walipa kodi wadogo na vipengele maalumu kama vilivyoainishwa katika Jadweli la Pili na Jadweli la Tatu la Sheria hii.

(3) Ushuru wa stempu utakuwa:

(a) kwa madhumuni ya kifungu cha 3(2)(a) na (b), kwa kiwango kitakachotozwa kwa mujibu wa thamani ya kodi;

(b) kwa hati zilizoainishwa chini ya aya ya (c) ya kifungu cha 3 (2), kwa kiwango kilichoainishwa katika Jadweli la Kwanza;

(c) kwa walipa kodi wadogo na vipengele maalumu vilivyoainishwa katika aya (d) itakuwa kwa kiwango kilichoainishwa katika Jadweli la Pili na Jadweli la Tatu.

(4) Bila ya kujali masharti ya Sheria hii, Waziri anaweza, baada ya kushauriana na Kamishna na kwa kuzingatia maslahi ya umma, kwa amri itakayochapishwa kwenye Gazeti Rasmi la Serikali, kuweka mgawanyo wa bidhaa au huduma ambazo zitakuwa na viwango maalumu visivyokuwa viwango vilivyoainishwa chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, kutumika kama ushuru wa stempu.

(5) Waziri anaweza, kwa amri iliyochapishwa kwenye Gazeti Rasmi la Serikali, kurekebisha, kuweka viwango vyengine na kutofautisha viwango vya ushuru wa stempu vilivyotajwa chini ya kifungu kidogo (3) (b) cha kifungu hiki.

(6) Ikiwa tozo la usambazaji wa bidhaa au huduma yoyote iliyomo ndani ya kifungu kidogo cha (2) (b) cha kifungu hiki kilichowekwa na kutozwa kodi chini ya Sheria ya Mafuta na Sheria ya Tozo la Huduma za Bandari, tozo la bidhaa au usambazaji litakuwa kwa mujibu wa Sheria husika.

Hati ya kutokuwa na pingamizi.

**4.** Bila kujali masharti ya Sheria inayohusiana na Uhaulishaji wa mali au hati ya umiliki, hakuna uhaulishaji wa mali yoyote au hati ya umiliki Zanzibar itakayotumiwa na mtu yeyote mpaka Kamishna awe ametoa hati ya kutokuwa na pingamizi.

Utawala.

**5.**-(1) Ushuru wa stempu utakaotozwa chini ya masharti ya Sheria hii na Sheria nyengine yoyote itakuwa chini ya usimamizi wa Sheria hii.

(2) Waziri anaweza, baada ya kushauriana na Kamishna, kwa amri itakayochapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali, kuteua mtu au tabaka la watu kuwa wakala au afisa aliyeidhinishwa kwa madhumuni ya Sheria hii kuhusiana na hati zote au mambo mengine yaliyoainishwa katika Sheria hii.

(3) Waziri anaweza, kwa kushauriana na Kamishna, kutengua uteuzi uliofanywa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

(4) Mtu aliyeteuliwa chini ya kifungu hiki atakuwa na wajibu wa kupokea fedha kuhusiana na kodi, au kukusanya kodi kwa njia za ushuru wa stempu na kulipa kiwango stahiki kwa Kamishna.

(5) Kwa madhumuni ya masharti ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Kamishna au mtu aliyeteuliwa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki kwa madhumuni ya ukusanyaji wa kodi, ataamua bei ya soko ya mali yoyote au hati inayostahiki kutozwa kodi.

(6) Mtu aliyeteuliwa ambae amezuia kinyume na utaratibu au kushikilia fedha alizopokea au kushindwa kukusanya kodi chini ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa.

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI YA JUMLA YANAYOHUSIKA NA HATI

Hati zinazo-stahiki kutozwa kodi.

**6.** Hati zifuatazo zitatozwa kodi kwa mujibu wa Jadweli la Kwanza:

(a) kila hati iliyoainishwa katika Jadweli la Kwanza ambayo awali haikutolewa na mtu, imetolewa Zanzibar na inahusiana na mali iliyopo, au kitu chochote kilichofanywa au kitakachofanywa Zanzibar;

(b) hati au waraka ulioandikwa au kutengenezwa nje ya Zanzibar na uliokubalika au uliolipwa, au uliowasilishwa kwa ajili ya kukubalika au

kulipiwa, au kuthibitishwa, kuhaulishwa au vyenginevyo kimakubaliano, ndani ya Zanzibar; na

(c) kila hati, isipokuwa hati ya malipo, hundi au hawala, iliyoainishwa katika Jadweli la Kwanza, ambayo haikutolewa kabla na mtu yeyote imetolewa nje ya Zanzibar, au kitu chochote kilichofanywa, au kitakachofanywa Zanzibar na kupokelewa Zanzibar.

Watu anayewajibika kulipa.

7.-(1) Watu waliotajwa katika Jadweli la Kwanza watawajibika kulipa ushuru wa stempu kwa hati zilizoainishwa ndani yake.

(2) Ikiwa kodi au adhabu zimelipwa chini ya Sheria hii na mtu kuhusiana na hati yoyote, na, kwa makubaliano au Sheria nyengine yoyote inayotumika wakati hati hiyo ilipokamilishwa, mtu mwengine aliwajibika kubeba gharama ya stempu stahiki kwa hati hiyo, mtu wa kwanza aliyetajwa atastahiki kurejesha gharama zake kutoka kwa huyo mtu mwengine kiwango cha kodi au adhabu iliyolipwa.

(3) Hakuna kilichomo ndani ya kifungu hiki kitakachozuiya makubaliano yoyote baina **ya** wahusika juu ya mgawanyo baina yao ya dhima ya kulipa kiwango cha kodi inayostahiki kutozwa.

(4) Isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo katika Sheria hii au Sheria nyengine inayotumika, mtu yeyote anaepaswa kulipa kodi kwa hati yoyote ambayo inapaswa kulipiwa kodi au ambaye atashindwa kulipa kodi hiyo kama inavyotakiwa na Sheria hii au kwa namna itakavyotumiwa hati isiyolipiwa ushuru wa stempu, atawajibika kulipa kodi hiyo mara mbili na atalipa ziada ya faini isiyozidi Shilingi Laki Tano.

Utambuzi.

**8.**-(1) Malipo ya ushuru, isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo katika Sheria hii, yatatambulika rasmi kwa kuwekwa stempu ya kubandikwa au stempu ya alama inayotozwa na kuoneshwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

(2) Endapo ushuru unaopaswa kulipwa au kuoneshwa kwa njia ya stempu ya kubandikwa, stempu hiyo itakuwa ni stempu ya mapato iliyotolewa chini ya Sheria hii kwa malipo ya ushuru wa stempu, ambao wakati ushuru unaotaka kulipwa au kuoneshwa, itakuwa ni stempu halali ya mapato.

(3) Kila stempu ya kubandikwa iliyotumika kuonesha malipo ya ushuru wa stempu chini ya Sheria hii, itafutwa haraka na mtu aliyeiweka kwa namna itakayoifanya isiweze kutumika tena kwa madhumuni ya kupata mapato yoyote.

(4) Ikiwa ushuru ambao hati inastahiki kutozwa itahitajika kuwekewa idadi kubwa ya stempu, risiti maalumu inaweza kutolewa kwa ushuru badala ya kuweka stempu, na kwa kutolewa risiti hiyo, afisa mapato au afisa aliyeidhinishwa atathibitisha hati ya cheti cha malipo yanayostahiki kulipwa ushuru huo, cheti ambacho kitajumuisha

nambari ya rejea na tarehe ya risiti iliyotolewa na kiwango cha ushuru uliolipwa kama ndio ushuru.

(5) Kila stempu iliyowekwa katika hati isiyokuwa hati iliyowekwa kielektroniki, itakuwa na viwango vitakavyoonesha tarehe halisi ambayo stempu iliwekwa.

(6) Waziri anaweza, kwa taarifa ya maandishi, kutangaza ushuru kuhusiana na hati yoyote au aina za hati utambuliwe kwa stempu ya alama au stempu ya kubandikwa na malipo ya ushuru, vyovyote yalivyo, yatatambuliwa ipasavyo.

Namna hati zitavyoandikwa na kuwekwa stempu.

**9.**-(1) Hati inayotozwa kodi ya ushuru wa stempu itaandikwa kwamba stempu inaweza kuonekana kwenye uso wa hati na haitaweza kutumika au kuwekwa katika hati nyengine yoyote.

(2) Hati inayotozwa kodi ya ushuru wa stempu inayojumuisha au inayohusiana na mambo mbali mbali itatozwa tofauti au kwa kila moja kama vile ni hati tofauti, ushuru wa stempu kwa kila mambo husika.

(3) Hati inayotozwa kodi ya ushuru wa stempu itawekwa stempu tofauti au kwa kila moja kwa ushuru wa stempu inayotozwa.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 8 cha Sheria hii, hati inayotayarishwa kwa makubaliano yoyote ambayo inatakiwa kutozwa ushuru wa stempu, na pia kwa makubaliano mengine yenye thamani, itatozwa ushuru wa stempu peke yake na tofauti, kama kwamba ni hati tofauti.

Adhabu kuhusiana na stempu ya kubandikwa.

**10.**-(1) Mtu ambaye kwa maandishi yoyote na kwa namna yoyote ameiharibu stempu ya kubandikwa kabla ya kutumika kwa lengo la kuonesha ushuru wa stempu atakuwa ametenda kosa na atatozwa faini isiyopunguwa Shilingi Laki Moja na isiyozidi Shilingi laki tano.

(2) Ikiwa mtu:

(a) kwa kudanganya ataondoa au atasababisha kuondolewa hati yoyote, stempu ya kubandikwa, au atabandika kwenye hati nyengine yoyote au kutumia kwa madhumuni mengine stempu nyengine yoyote ya wazi ambayo imetolewa kwa madhumuni stempu hiyo kuweza kutumika tena; au

(b) anauza, au anakusudia kuuza, au anatangaza, stempu yoyote ya kubandikwa ambayo imeondolewa, au anatangazia hati yoyote iliyo na stempu ya kubandikwa ambayo anajuwa kuwa imeondolewa;

atakuwa ametenda kosa, pamoja na ziada ya faini au adhabu nyengine, ambazo zinamuwajibikia, atatozwa faini isiyopunguwa Shilingi Laki Moja na isiyozidi Shilingi Laki Tano.

Uwekaji wa stempu kwa baadhi ya hati.

**11.**-(1) Waziri anaweza, kwa amri itakayochapishwa kwenye Gazeti Rasmi la Serikali, kuweka masharti ya ulipaji wa kodi kwa hati zozote zilizoainishwa katika Jadweli la Kwanza kwa kutumia mashine inayoweka bei ya stempu.

(2) Kila muhuri unaoonesha malipo ya kodi yaliyofanywa kwa kupitia mashine ya kuwekea bei ya stempu unaotumika kwa kibali cha leseni chini ya kifungu hiki utakuwa na tarehe sahihi ya kuweka muhuri huo.

(3) Uwekaji wa stempu kwa hati yoyote chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kwa mtu yoyote aliyepewa mamlaka kama ilivyotajwa kwenye kifungu hiki, ikiwa itafanyika kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki na ya leseni, athari yake itakuwa ni sawa kama ufutwaji wa stempu ya kubandikwa kwa tarehe na tathmini iliyooneshwa na mashine ya kuwekea muhuri.

Uchunguzi na uzuiaji wa hati.

**12.**-(1) Maelezo yote na mazingira yanayoathiri dhima ya hati kulipiwa kodi au kiwango cha kodi ambacho kwa kila hati kinatozwa, yanatakiwa yawe kamilifu na sahihi kama ilivyotajwa katika hati, na afisa aliyeidhinishwa anaweza kuhitaji ushahidi huo kupatikana kama itakavyohitajika kuthibitisha kwamba maelezo yote na mazingira yamewekwa sahihi.

(2)Afisa aliyeidhinishwa anaweza kuzuia hati ambayo haijakamilisha maelezo yote na mazingira yanayoathiri dhima ya hati hiyo kulipiwa kodi au kiwango cha kodi ambacho hati hiyo inatozwa kodi.

(3) Iwapo hati imepelekwa kwa Afisa aliyeidhinishwa chini ya Sheria hii, kwa maoni ya Afisa aliyeidhinishwa ni:

(a) moja ya maelezo yake inastahiki kulipiwa kodi na afisa huyo ameona kwamba kodi tayari imeshalipwa; au

(b) kodi iliyoamuliwa na Afisa huyo au kiwango hicho, baada ya kodi kulipwa, malipo hayo ni sawa na kodi iliyoamuliwa,

afisa huyo atathibitisha kwa maelezo katika hati hiyo yanayoainisha kiwango, ambacho kinastahiki kutozwa kimelipwa.

(4) Hati ambayo uthibitishwaji wake umefanywa chini ya kifungu hiki:

(a) itachukuliwa kuwa imewekwa stempu sahihi au haitatozwa kodi, kama itakavyokuwa; na

(b) ikiwa itatozwa kodi, itapokelewa katika ushahidi au vyenginevyo, na inaweza kufanyiwa kazi na kusajiliwa kama kwamba iliwekwa stempu sahihi.

(5) Endapo afisa aliyeidhinishwa atazuia hati chini ya kifungu hiki au atapokea hati iliyopelekwa kwake isiyotozwa kodi au hati ya malipo au hawala, na kwa maoni yake kwamba hati hiyo inatozwa kodi na haijawekwa stempu ipasavyo, atahitaji malipo sahihi au kiwango kinachohitajika kulipiwa kodi, pamoja na adhabu itakayoelezwa.

(6) Mtu ambaye ana lengo la kukwepa malipo ya kodi:

(a) anatoa hati ambayo maelezo yote na mazingira yaliyomo hayajakamilika na si sahihi; au

(b) ameajiriwa au anahusika au yumo katika kutayarisha hati yoyote ameshindwa kuweka maelezo yote au mazingira sahihi;

atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua Shilingi Laki moja lakini isiyozidi Shilingi Laki Tano.

Ufutwaji wa stempu.

**13.**-(1) Stempu zilizotumika katika hati zozote zilizoelezwa katika Jadweli la Kwanza zitakapowekwa zitakuwa na muhuri maalumu unaoonesha tarehe ya kutolewa hati hiyo.

(2) Endapo ushuru wa stempu utahitajika au kuruhusiwa na Sheria yoyote kwa ajili ya kuonesha stempu ya kubandikwa, stempu itafutwa kwa namna ya kuifanya isiweze kutumika tena kwa ajili ya mapato yoyote.

(3) Hati yoyote inayoonesha stempu isiyokamilisha matakwa ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki au haijafutwa kwa namna ilivyoelezwa katika kifungu hiki, ambapo hati hiyo inahusika, itachukuliwa kama haijawekwa stempu.

(4) Stempu zilizotumika katika hati za aina yoyote zinaweza kufutwa katika stempu yoyote iliyowekwa au waraka uliopendekezwa kuandikwa, utakaofuatwa, kwa kuwekwa neno "kufutwa" na "muhuri maalumu", sahihi ya afisa na tarehe iliyoandikwa au kuchapishwa sehemu kwenye stempu na sehemu kwenye waraka ambao stempu imewekwa ama stempu yote au sehemu ya stempu au sehemu ya waraka ambao stempu imewekwa, na kwamba stempu hiyo haiwezi kutumika tena.

(5) Endapo stempu mbili au zaidi zitatumika kuashiria ushuru wa stempu katika hati yoyote, kila stempu itafutwa kwa namna ilivyoelezwa katika kifungu hiki.

(6) Endapo hati ya ushuru wa stempu ambayo inahitajika au kuruhusiwa na Sheria yoyote kuashiria stempu ya kubandika.

(a) itawekwa stempu kabla ya kukamilishwa au kabla ya kutolewa, au kabla ya kuwekwa alama, au kabla ya kufanya jambo lolote;

(b) mtu wa mwanzo anayekamilisha au mtu anayeitoa, au mtu anayeweka alama katika hati, au mtu anayefanya jambo hilo kama itakavyokuwa, atafuta stempu ya kubandikwa kabla hajaweka au kabla ya kuzitoa katika hati au kabla ya kufanya jambo lolote, kama itakavyokuwa.

(7) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ikiwa wakati hati ya malipo au hawala zipo katika mikono ya mhusika Zanzibar:

(a) stempu sahihi itawekwa katika hati na itafutwa kwa namna itakavyoelezwa; na

(b) mhusika hana sababu ya kuamini kwamba stempu iliwekwa au itafutwa isipokuwa na mtu na kwa wakati unaohitajika na Sheria hii,

Stempu inayohusiana na mhusika huyo, itachukuliwa imewekwa na imefutwa.

(8) Masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki hayatamsamehe mtu kutokana na adhabu iliyosababishwa na yeye kwa kuacha kuweka au kufuta stempu.

(9) Mtu ambaye atadharau au atakataa kufuta kikamilifu stempu ya kubandika kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki atakuwa ni mkosa na atatozwa faini isiyozidi Shilingi Laki Tano.

Ufutaji kwa mawakala walioteuliwa.

**14.**-(1) Endapo hati imetolewa na wakala aliyeidhinishwa ikiwa chombo kinachojitegemea au chombo kwa kiasi fulani kinachojitegemea, ufutwaji utachukuliwa umefanywa kwa usahihi ikiwa umefanywa kwa namna ilivyoelezwa na kwa muhuri au alama kwa kutumia wino jina kamili la shirika au herufi za mwanzo za jina hilo au herufi za mwanzo za jina la meneja, katibu au mtu mwengine anayetoa hati hiyo kwa niaba ya chombo pamoja na tarehe husika kama ilivyoelezwa.

(2) Mtu anayetakiwa na Sheria kufuta stempu ya kubandikwa, atadharau au atakataa kufanya hivyo kwa namna ilivyoelezwa atakuwa ametenda kosa na atatozwa faini isiyozidi Shilingi laki Tatu.

Thamani ya mali inayostahiki kulipiwa kodi.

**15.**-(1) kwa masharti ya kifungu hiki, thamani ambayo kodi inalipwa, itakuwa kiwango cha makubaliano kinacholipwa na malipo kwa mtu ambaye amepata mali hiyo au ikiwa hakuna kiwango kilichokubalika kulipwa, itakuwa ni wastani wa thamani ya soko ya mali.

(2) Ikiwa muamala mmoja wa mali umebadilika kwenda kwa mwengine na hakuna malipo ya ziada yatakayolipwa na upande wowote wa muamala huo, thamani

ushuru unaolipwa kuhusiana na kupata kwa kila mali utakuwa ni wastani wa thamani ya soko ya kila mali.

(3) Ikiwa mali zilizobadilishwa hazikuwa na thamani sawa, ushuru, kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, utalipwa kuhusiana na upatikanaji wa kila mali kwa wastani wa thamani ya soko ya mali ambayo ina thamani kubwa.

(4) kwa mauziano ambayo mali moja itabadilishwa na nyengine na malipo ya ziada yatalipwa na upande wowote kwa mauziano hayo, thamani ambayo ushuru utalipwa kwa mujibu wa kifungu hiki itakuwa:

(a) kwa upatikanaji wa mali ambayo malipo ya ziada yamelipwa, utakuwa wastani wa thamani ya soko ya mali hiyo, au wastani wa thamani ya soko ya mali iliyobadilishwa kwa mali hiyo pamoja na malipo ya ziada yatakayolipwa, kwa yoyote iliyo kubwa ; na

(b) kwa upatikanaji wa mali nyengine, utakuwa wastani wa thamani ya soko ya mali hiyo, au wastani wa thamani ya mali iliyotolewa kwa kubadilishwa na mali hiyo ukitoa malipo ya ziada yatakayolipwa kwa yoyote iliyo kubwa.

(5) Masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki hayatatumika kwa upatikanaji wa mali iliyouzwa kwa mnada, isipokuwa afisa aliyeidhinishwa ameridhika kwamba mauzo hayo hayakuwa mauzo ya nia njema kupitia mnada, au kuna njama baina ya muuzaji na mnunuzi, au wakala wao.

(6) Endapo mali itahaulishwa baina ya pande zenye mahusiano, thamani ya mali itaamuliwa kwa kiwango kinachokubalika.

Maelekezo kuhusiana na ushuru wa baadhi ya hati za uhaulishaji mali.

**16.**-(1) Endapo mali imeingiwa mkataba wa kununuliwa kwa malipo ya pamoja kwa mali yote kwa watu wawili au zaidi kwa pamoja, na hati hiyo imetozwa kodi tofauti na kwa kila moja kama ni hati moja, stempu hiyo itachukuliwa kuwa ni hati tafauti.

(2) Endapo mtu:

(a) ameingia mkataba wa kununua mali yoyote lakini hajapata hati ya kuhaulisha mali, na akaamua kuingia mkataba kumuuzia mtu yeyote; na

(b) amehaulisha mali kwa mnunuzi mwengine.

uhaulishaji utatozwa ushuru kwa kuzingatia malipo ya mauzo kutoka kwa mnunuzi wa awali kwenda kwa mnunuzi mwengine.

(3) Endapo mtu ataingia mkataba wa kununua mali lakini hakuwa na hati ya uhaulishaji wa mali, ataingia mkataba wa kuuza mali yote au sehemu ya mali hiyo kwa mtu mwengine yeyote na mali iliyohaulishwa na muuzaji wa awali kwa watu tofauti kwa kila sehemu, uhaulishaji wa kila sehemu iliyouzwa kwa mnunuzi mwengine utatozwa ushuru kwa mujibu wa malipo yaliyolipwa na mnunuzi mwengine bila ya kuzingatia kiwango au thamani ya malipo ya mwanzo.

(4) Uhaulishaji wa mali iliyobaki kwa muuzaji wa awali, kama ipo, utatozwa ushuru kwa mujibu wa kilichozidi kwa malipo ya awali juu ya malipo ya jumla yaliyolipwa na wanunuzi wengine.

Sehemu au upande.

**17.**-(1) Endapo sehemu au upande wowote wa jengo, mali, malipo yoyote yanayolipwa au kutolewa au yanayokubalika kulipwa au kutolewa kwa usawa, malipo au hati ambayo sehemu au upande huo utatozwa ushuru kwa kiwango cha asilimia sawa ya ushuru kulingana na thamani ya ushuru wa mauzo kwa malipo hayo na kwa ushuru huo tu.

(2) Endapo zaidi ya mali moja inahusiana na muamala huo huo, kiwango cha ushuru kinacholipwa kinachohusiana na kila mali kitahesabiwa kwa thamani ya mali hiyo kama kwamba mali hiyo ilikuwa ni mauziano tofauti.

Hati za Uingizaji na usafirishaji wa bidhaa.

**18.** Mtu ambaye anatayarisha au anatoa hati yoyote ya uingizaji au usafirishaji bidhaa ambayo haijawekwa stempu atakakuwa ametenda kosa na atatozwa faini isiyopungua Shilingi Laki Mbili na isiyozidi Shilingi Laki Tano.

Hati ya malipo na hawala.

**19.**-(1) Hati ya malipo au hawala iliyotayarishwa na kukusudiwa kulipwa papo hapo au kwa kuiwasilisha, kwa madhumuni ya Sheria hii, itachukuliwa kuwa ni hati ya malipo au hawala inayolipwa itakapohitajika.

(2) Ushuru unaotozwa unaohusiana na hati za malipo au hawala, kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, unaweza kutambuliwa kwamba ni stempu za kubandikwa zilizowekwa au zinazoweza kuwekwa sehemu ya hati hizo kwa stempu za wazi na sehemu nyengine kuwekwa stempu za alama.

(3) Endapo hati ya malipo inatayarishwa kwa seti kwa mujibu wa wafanya biashara na ikiwa seti imewekwa stempu sahihi, seti nyengine, isipokuwa zimetolewa katika utaratibu au imekubaliwa kwa sehemu inayotokana na hati iliyowekewa stempu hiyo ya ushuru ambayo haikutolewa au katika namna imekubaliwa kwa sehemu kwa namna yoyote imekubaliwa mbali ya kupotea au kuharibika, hata kama haijawekwa stempu, itakubaliwa katika ushahidi utakaothibitika maelezo ya hati iliyopotea au hati iliyoharibiwa.

(4) Hati ya malipo au hawala ambayo inakusudiwa kutayarishwa au kutengenezwa nje ya Zanzibar, kwa madhumuni ya kutathimini utaratibu ambao ushuru wa stempu utatambuliwa, itachukuliwa kuwa hati hiyo imetayarishwa au imetengenezwa, ijapokuwa inaweza kiuhalisia kutayarishwa au kutengenezwa ndani ya Zanzibar.

Uhaulishaji kwa njia ya mauzo.

**20.**-(1) Hati ambayo mali imehaulishwa kisheria au kwa usawa au amekabidhiwa mtu mwengine kwa njia ya kubadilishana itachukuliwa imehaulishwa kuwa ni uhaulishaji wa mauzo ya mali hiyo kwa njia ya mauziano na ushuru wa stempu utatathminiwa na kulipwa ipasavyo.

(2) Endapo makubaliano au sehemu ya makubaliano ya uhaulishaji kuhusiana na mauzo yatajumuisha:

(a) dhamana ya soko, uhaulishaji huo utatozwa kwa mujibu wa kiwango cha ushuru kwa asilimia kwa kuzingatia thamani ya dhamana hiyo;

(b) dhamana yoyote isiyokuwa na dhamana ya soko, uhaulishaji huo utatozwa kwa kiwango cha ushuru kwa asilimia kwa kuzingatia kiwango kinachostahiki kulipwa kwa siku na tarehe kwa kiwango halisi na riba.

Tathmini ya malipo kwa vipindi.

**21.**-(1) Endapo hati inatolewa kudhamini malipo ya mwaka au kiwango kingine kinalipwa kwa vipindi, au endapo makubaliano ya uhaulishaji ni ya mwaka au yatalipwa kiwango kingine kinalipwa kwa vipindi, kiwango cha hati kilichodhaminiwa katika hati au makubaliano ya uhaulishaji kama itakavyokuwa, kwa madhumuni ya Sheria hii, itazingatiwa kuwa:

(a) endapo kiwango kinacholipwa kwa kipindi maalum kitapelekea kiwango chote kinachotakiwa kulipwa kuweza kuthibitishwa kabla, uhaulishaji huo utatozwa kwa mujibu wa makubaliano hayo kwa kiwango cha ushuru kwa asilimia ya malipo hayo ya jumla;

(b) endapo kiwango kinacholipwa si cha kudumu au hakina kipindi maalum cha ukomo kwa kipindi chote kitakachokuwa katika tarehe ya hati au uhaulishaji, kiwango chote, kwa mujibu wa masharti ya hati au uhaulishaji kinaweza kulipwa katika kipindi cha miaka kumi na tano kitakachohesabiwa kutoka tarehe ambapo malipo ya mwanzo yanafanyika; na

(c) endapo kiwango kinalipwa kwa kipindi kisichokuwa maalum cha ukomo cha maisha yoyote ikiwa kwa tarehe ya hati au uhaulishaji,

kiwango cha juu ambacho kinaweza kulipwa kama ilivyoelezwa katika aya ya (b) katika muda wa miaka kumi kitahesabiwa kutoka tarehe ambayo malipo ya mwanzo yalipaswa kulipwa.

(2) Hakuna uhaulishaji wa mauzo unaotozwa kwa kiwango cha ushuru kwa asilimia kulingana na malipo ya vipindi na kuingiza pia sharti la kudhamini malipo ya vipindi hivyo utakaotozwa ushuru wowote vyovyote iwavyo kulingana na masharti hayo, na hakuna hati tafauti zilizotengenezwa katika njia nyengine kwa kudhamini malipo ya vipindi itatozwa kwa kiwango cha juu cha ushuru kisichozidi Shilingi Laki Moja.

Athari ya maelezo ya thamani.

**22.**-(1) Endapo hati inajumuisha maelezo ya kiwango kilichopo cha kubadilishia fedha au bei iliyowekwa au wastani wa thamani na kuwekwa stempu kwa mujibu wa maelezo hayo, kwa kuzingatia kiini cha maelezo hayo, itachukuliwa imewekwa stempu sahihi.

(2) Afisa aliyeidhinishwa au wakala aliyeteuliwa chini ya Sheria hii atatakiwa kuthibitisha maelezo ya kiwango kilichopo cha kubadilisha fedha kabla ya kuweka stempu hati yoyote iliyowasilishwa kwake.

(3) Ikiwa maelezo hayo yatathibitika kuwa siyo sahihi, utofauti wa ushuru na faini utagombolewa.

(4) Mtu atakayeshindwa au atakayekataa kufuata uthibitisho wa afisa aliyeidhinishwa au wakala chini ya kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa na atatozwa faini isiyozidi Shilingi Laki Tano.

Namna ya kuhesabu kiwango cha ushuru kwa asilimia.

**23.**-(1) Endapo hati inatozwa kiwango cha ushuru kwa asilimia kwa mujibu wa-

(a) kiwango chochote kwa fedha yoyote ya kigeni ; au

(b) dhamana ya hisa yoyote au soko,

ushuru utahesabiwa, katika siku ya tarehe ya hati, kwa thamani ya fedha kwa mujibu wa kiwango kilichopo cha kubadilishia fedha, au hisa au dhamana kwa mujibu wa wastani wa bei iliyopo.

(2) Endapo hati inajumuisha maelezo ya kiwango kilichopo cha kubadilishia fedha, au wastani wa kiwango cha kubadilishia fedha au wastani wa bei kama itakavyohitajika, na imewekwa stempu kwa mujibu wa maelezo hayo, kwa kuzingatia kiini cha maelezo, itachukuliwa imewekwa stempu sahihi, isipokuwa au hadi itakavyoonekana kwamba maelezo hayo siyo ya kweli, na hati hiyo kiuhalisia haikutimiza masharti ya kuwekwa stempu.

Uhaulishaji wa makubaliano ya deni au malipo ya baadae kutozwa.

**24.**-(1) Endapo mali yote au sehemu ya mali inahaulishwa kwa mtu kwa makubaliano ya kulipa deni kwa mtu huyo, au kinachouzwa kinafahamika au hakifahamiki kwa malipo au uhaulishaji wa fedha au hisa, ama kipo au kinapelekea kutozwa au kutokufahamika kuhusiana na mali au vyenginevyo, deni, fedha au hisa kwa kuzingatia makubaliano itachukuliwa yote au sehemu, kama itakavyokuwa, kwamba uhaulishaji unatozwa ushuru.

(2) Kuhusiana na mauzo ya mali iliyowekwa rehani au kizuizi chengine, rehani yoyote ya fedha isiyolipwa au fedha iliyotozwa, pamoja na riba, kama itakuwepo, iliyowekwa kizuizi hicho, itachukuliwa ni sehemu ya makubaliano ya mauzo.

(3) Endapo mali iliyowekwa rehani imehaulishwa kwa muwekewa rehani, muwekewa rehani atastahiki kukata kutoka katika ushuru unaolipwa kuhusiana na uhaulishaji, kiwango cha ushuru kilicholipwa kuhusiana na rehani.

Rehani.

**25.**-(1)Katika kutathmini kiwango cha ushuru wa stempu kinacholipwa kwa madhumuni ya uhaulishaji wa rehani kwa namna itakavyotajwa, masharti yafuatayo yatafuatwa:

(a) Endapo uhaulishaji wowote wa rehani utafanywa kwa uteuzi wa mdhamini au wadhamini chini ya wasia, usuluhishi au hati nyengine au kwa amri ya Mahkama, ushuru kwa uhaulishaji huo utakuwa kama ilivyoelezwa katika Jadweli la Kwanza.

(b) Endapo uhaulishaji wowote wa rehani unaonesha kuwa uhaulishaji huo unafanywa au unatekelezwa kwa njia ya ukamilishaji au uthibitishaji wa hati ya umiliki na hakuna sababu nyengine au endapo uhaulishaji huo unaonesha kuwa hakuna maslahi atakayoyapata mtu anayefaidika na uhaulishaji huo unaofanywa au unaotekelezwa au kwamba hakuna maslahi makubwa anayoyapata mtu huyo au anastahiki kuwa nayo kwa mujibu wa sheria au kwa sababu ya hati nyengine, ushuru wa uhaulishaji huo utakuwa kama ulivyoelezwa katika Jadweli la Kwanza.

(2) Hakuna katika kifungu hiki kitakachochukuliwa kusamehe uhaulishaji wowote wa rehani kutoka kwenye dhima kwa ushuru mwengine wowote ambao unapaswa au unalazimika chini ya sheria hii au sheria nyengine yoyote inayohusiana na ushuru wa stempu.

Uhaulishaji wa hiari.

**26.**-(1) Uhaulishaji unaofanywa kwa hiari utatozwa ushuru wa stempu kama umehaulishwa kwa njia ya mauzo.

(2) Uhaulishaji, usiokuwa umefanywa kwa maslahi ya mnunuzi au aliyeweka kizuizi au mtu mwengine kwa nia njema na kwa makubaliano ya thamani ya malipo, kwa madhumuni ya kifungu hiki, utachukuliwa ni uhaulishaji unaofanyika kwa hiari, na isipokuwa endapo makubaliano yanahusiana na ndoa, makubaliano ya uhaulishaji wowote hayatachukuliwa kwa madhumuni haya kuwa ni makubaliano ya thamani ya malipo kwa sababu ya kutojitosheleza kwa kiwango kilicholipwa kama makubaliano au kwa mazingira mengine ya uhaulishaji utakuwa na maslahi makubwa kwa mtu ambaye mali imehaulishwa kwake.

(3) Uhaulishaji uliofanywa kwa makubaliano ya kawaida kwa madhumuni ya kudhamini malipo mengine ya awali au mkopo au uliofanywa kwa madhumuni ya uteuzi wa mdhamini mpya au kumaliza muda kwa mdhamini, ikiwa udhamini umeelezwa au unajieleza kivitendo au ambapo hakuna maslahi yaliyotolewa kwa mali iliyohaulishwa, au umefanywa kwa maslahi ya mdhamini au mtu mwengine yeyote mwenye uwezo wa kifedha katika udhamini wowote, ikiwa umeelezwa au unajieleza kivitendo, hautatozwa ushuru chini ya kifungu hiki.

Namna itakavyotozwa dhamana kwa malipo ya baadae.

**27.**-(1) Dhamana ya malipo au malipo ya marejesho ya fedha zitakazokopeshwa, malipo ya awali au yaliyolipwa, au ambayo yatakamilika kupitia akaunti ya muda, ikiwa ilikuwa na fedha au haikuwa na fedha kabla, itatozwa, iwapo kiwango chote kimedhaminiwa au kitalipwa kwa njia yoyote ya ukomo, kwa ushuru unaofanana kama dhamana kwa kiwango cha ukomo.

(2) Endapo kiwango chote hicho si cha ukomo, dhamana itakuwepo kwa kiwango kitakachowekwa stempu kwa asilimia ya ushuru inayopelekea kufidia; lakini endapo malipo ya awali au mkopo umefanywa katika zaidi ya kiwango kilichofidiwa kwa ushuru huo, kwa madhumuni ya ushuru wa stempu, dhamana itachukuliwa kuwa ni mpya na hati tafauti inayoainisha tarehe ya siku ambayo malipo ya awali au mkopo umefanywa.

(3) Hakuna fedha zitakazolipwa awali kwa bima ya mali yoyote iliyojumuishwa katika dhamana dhidi uharibifu wa moto, au kwa kuweka sera yoyote ya bima ya maisha inayojumuisha dhamana, au itakayoathiri ndani yake sera mpya ya bima, itazingatiwa kama ni sehemu ya kiwango kinachohusiana na dhamana inayotozwa kwa kiwango cha ushuru kwa asilimia.

Namna ya ukodishaji kutozwa mrahaba.

**28.** Endapo makubaliano ya ukodishaji yote au sehemu, mrahaba utalipwa ama fedha, uzalishaji au bidhaa au makubaliano mengine yoyote ilivyo mbali ya kiwango cha fedha, ikiwa, itaainishwa kwamba kiwango cha fedha hizo au thamani ya uzalishaji au bidhaa hizo kimefikia kwa uchache, au hakizidi kiwango kilichotolewa, au endapo mkodishwaji ametozwa kiwango maalum au kina mbadala wa malipo baada

ya kiwango maalum cha kubadilisha fedha, kiwango cha mwaka cha fedha hizo na thamani ya uzalishaji au bidhaa hizo kitakadiriwa katika kiwango hicho kilichotolewa au kwa mujibu wa kiwango kilichotolewa.

Ushuru wa ukodishaji kwa mazingira **mengineyo.**

**29.** Ukodishaji, iwapo makubaliano yamejumuisha malipo au makubaliano mengine mbali na ukodishaji, yanamhusu ama mkodishaji au mtu mwengine yeyote, utatozwa kwa kiwango cha ushuru kwa asilimia kilichohesabiwa kuhusiana na makubaliano kama kwamba ni uhaulishaji kuhusiana na mauzo kwa kiwango cha makubaliano hayo.

Namna ya kutoza ukodishaji katika uzalishaji au vyenginevyo.

**30.**-(1) Endapo makubaliano au sehemu ya makubaliano ambayo ukodishaji wowote umefanywa au umekubaliwa kufanywa haujumuishi fedha lakini unajumuisha uzalishaji wowote au bidhaa nyengine, ushuru utahesabiwa katika thamani ya uzalishaji huo au bidhaa hizo katika makubaliano au wastani wa bei ya soko iliyopo katika tarehe ya hati.

(2) Endapo imeelezwa kwamba thamani ya uzalishaji au bidhaa una kiwango kidogo, au hauzidi kiwango kilichotolewa, au iwapo mkodishaji anatozwa pekee na au ana mbadala wa kulipa baada ya kiwango maalum cha kubadilisha fedha, thamani ya uzalishaji au bidhaa, kwa madhumuni ya kutathmini kiwango cha ushuru kwa asilimia, itakadiriwa katika kiwango kinachotowa, au kwa mujibu wa kiwango kilichopo.

(3) Ukodishaji au makubaliano ya ukodishaji yaliyofanywa ama yote au sehemu ya malipo, ikiwa imejumuisha maelezo ya thamani, na imewekewa stempu kwa mujibu wa maelezo, kwa kuzingatia kiini cha maelezo, utachukuliwa kuwa umewekwa stempu sahihi, isipokuwa au hadi itakavyoonesha vyenginevyo kwamba maelezo hayo sio sahihi, na kwamba ukodishaji au makubaliano kiuhalisia hayajawekewa stempu sahihi.

Ushuru katika ukodishaji wenye kodi tofauti.

**31.** Inapotokea ukodishaji una kodi iliyoelezwa kwa kipindi maalum kinachoelezwa au kwa vipindi pamoja na masharti ya kukodi tena kwa kipindi hicho cha mwisho yamewekwa kwa kutathminiwa au vyenginevyo, ushuru utatathiminiwa katika kodi ya juu iliyowekwa katika ukodishaji huo, na ikiwa kodi mpya itakapowekwa kwa kutathminiwa au vyenginevyo kama ilivyoelezwa itazidi kodi ambayo ilikadiriwa ushuru mwanzoni, ushuru ulioongezeka utalipwa na hati ya ukodishaji itawasilishwa kwa kutathminiwa ipasavyo kwa namna na kwa madhumuni ya masharti hayo kama faini na vyenginevyo kama ilivyojitokeza katika tathmini ya awali.

Hati hazitathibitishwa kwa kiapo mpaka ziwekwe stempu.

**32.**-(1) Kila Muapishaji ambaye kwa kujua na kwa hiari kwa kitendo cha kuapisha anashuhudia au anathibitisha utekelezaji wa hati yoyote inayopaswa kutozwa ushuru na ikadhihirika kutokuwekwa stempu sahihi atakuwa ametenda kosa na atatozwa faini isiyopungua Shilingi Laki Mbili na isiyozidi Shilingi Laki Tano.

(2) Hakuna katika Sheria hii kitakachopelekea muapishaji kuwa na dhima ya kulipa faini kwa sababu za kushuhudia kwake utolewaji wa hati yoyote kwa sababu tu ni shahidi na bila ya kuweka, kuambatanisha au kulipia kitendo cha kuapisha.

Sera za bima.

**33.**-(1) Endapo kufanywa upya kwa sera yoyote ya bima inayopaswa kutozwa ushuru imeathiriwa na malipo ya awali, risiti ya malipo ya awali itatolewa na kuwekwa stempu kwa thamani halisi ya ushuru unaolipwa kwa kufanywa upya.

(2) Mtu ambaye:

(a) anapokea au anachukua madai ya malipo ya awali au makubaliano kwa sera yoyote ya bima au kufanywa upya kwa sera hiyo inayopaswa kutozwa ushuru na haikufanywa, ndani ya mwezi mmoja baada ya kupokea au kuchukua madai kwa malipo hayo ya awali au makubaliano, yatafanywa na kutekeleza sera sahihi iliyotozwa stempu halisi, risiti au hati; au

(b) analipa au anaruhusu katika hesabu ya benki, au anakubali kulipa au kuruhusu katika hesabu ya benki, fedha yoyote au kuhusiana na sera yoyote ya bima au sera hiyo inayofanywa upya ambayo haikuwekwa stempu sahihi.

ataadhibiwa chini ya Sheria hii.

(3) Endapo ushuru wowote wa stempu ulioongezeka utalipwa katika sera ya bima baada ya utekelezaji, malipo ya ushuru huo yanaweza kutambuliwa kwa kuwekwa stempu katika sera au kwa kuthibitisha au hati nyengine ambayo inaeleza mazingira ya kutoa ongezeko la ushuru huo au kwa risiti yoyote inayothibitisha malipo yoyote ya awali.

Sera ya bima ya usafiri wa bahari.

**34.**-(1) Kutatozwa ushuru kuhusiana na bima ya usafiri wa bahari inayojumuisha sharti la kuendelea, utozaji wa ushuru wa stempu kama ilivyotajwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria hii na zaidi ya ushuru wa stempu ambao ni mwengineo, hutozwa kuhusiana na sera.

(2) Sera ya bima ya usafiri wa bahari haitakuwa halali isipokuwa iwe imeainisha taarifa za vihatarishi au athari au muda ambao sera hiyo inafanywa, majina ya wapokeaji au walengwa na kiwango au viwango vilivyowekewa bima.

(3) Endapo sera yoyote ya bima ya usafiri wa bahari imefanywa kwa au kuhusiana na safari na pia kwa muda, au kuongezwa au kufidia muda wowote uliozidi siku thelathini baada ya meli kuwasili katika kituo chake na ikafunga gati, sera itatozwa ushuru kama sera kwa au kuhusiana na safari na pia itatozwa ushuru kama sera kwa muda.

(4) Bila ya kujali chochote kilichopo katika kifungu hiki, sera ya bima ya usafiri wa bahari iliyofanywa kwa muda inaweza kuingiza sharti la kuendelea, na sera hiyo haitakuwa si halali kwa msingi tu kwamba sababu ya sharti la kuendelea linaweza kupelekea kuwepo kwa kipindi kilichozidi miezi kumi na mbili.

(5) Ikiwa vihatarishi vimefidiwa na sharti la kuendelea lililoeleza, na sera mpya haijatolewa kufidia vihatari, sharti la kuendelea litachukuliwa kuwa ni jipya na mkataba tafauti wa bima ya usafiri wa bahari ulioelezwa katika sera ambayo imejumuishwa, lakini haikufidiwa kwa kuwekwa stempu na sera itawekwa stempu kwa madhumuni ya mkataba huo ipasavyo, lakini inaweza kuwekewa stempu bila ya adhabu katika muda wowote usiozidi siku thelathini baada ya vihatarishi kuelezewa.

(6) Endapo mtu yeyote, kwa makubaliano ya kiwango chochote cha fedha kilicholipwa au kitakacholipwa kwa usafirishaji wa ziada au vyenginevyo, akakubali yeye mwenyewe kuchukua kihatarishi chochote kuhusiana na bidhaa, biashara au mali yenye maelezo yeyote yalivyo wakati wa usafirishaji katika meli au chombo cha baharini, au kumfidia mmiliki wa bidhaa hizo, biashara au mali kutokana na kitaharishi chochote, upotevu au hasara, makubaliano au mapatano hayo yatachukuliwa kuwa ni mkataba wa bima ya usafiri wa bahari.

Mkataba wa ukodishaji chombo cha usafiri.

**35.**-(1) Ushuru unaohusiana na mkataba wa ukodishaji wa chombo cha usafiri baharini na angani unaweza kutambuliwa na stempu ya kubandikwa ambayo itawekwa na kufutwa katika muda wa utekelezaji kwa mtu ambaye hati hiyo alipaswa kuitekeleza kwa mara ya kwanza.

(2) Ushuru unaohusiana na mkataba wa ukodishaji wa chombo cha usafiri baharini na angani utatambuliwa na stempu ya kubandikwa ambayo itafutwa na mtu ambae hati hiyo imetekelezwa kwake kwa mara mwisho au utekelezaji wake umekamilishwa kama sharti la mkataba uliofungwa.

(3) Endapo mkataba wa ukodishaji wa chombo cha usafiri baharini na angani ambao haujawekwa stempu sahihi unatekelezwa kwa mara ya kwanza nje ya Zanzibar, upande wowote wa mkataba huo unaweza, ndani ya siku saba baada kupokelewa kwa mara ya kwanza na kabla haujatekelezwa na mtu yeyote ndani ya Zanzibar, kuweka stempu ya wazi inayotambua ushuru unaotozwa na wakati huo huo kufuta stempu ya wazi, na hati itachukuliwa imewekwa stempu sahihi.

(4) Mkataba wa ukodishwaji wa chombo cha usafiri baharini na angani unaweza kuwekewa stempu na Kamishna baada ya utekelezaji na kwa sharti kwamba:

(a) ndani ya siku saba baada ya utekelezaji kwa mara ya kwanza kutolewa malipo ya ushuru na faini ya Shilingi Laki Moja.

(b) baada ya siku saba baada ya utekelezaji kwa mara ya kwanza kutolewa malipo ya ushuru na faini Shilingi Laki Mbili.

Kuwekwa stempu makubaliano ya ukodishaji kwa madhumuni ya kununua.

**36.** Makubaliano ya au yanayohusiana na usambazaji wa bidhaa zinazokodishwa, ambapo bidhaa hizo zinamakubaliano ya malipo ya vipindi yanaweza kuwa mali ya mtu ambaye amepelekewa, yatatozwa ushuru kama makubaliano au, kama ikiwa chini ya masharti, yatakuwa kama hati, kama itakavyokuwa.

Utiaji thamani hisa na dhamana za soko.

**37.**-(1) Endapo hati inatozwa ushuru kuhusiana na hisa au dhamana yoyote ya soko au dhamana nyengine, ushuru utahesabiwa katika thamani ya hisa au dhamana kwa mujibu wa wastani wa bei au thamani ya hisa au dhamana kwa tarehe ya hati hiyo.

(2) Endapo hati inatozwa ushuru kwa kiwango cha asilimia kulingana na dhamana yoyote ya soko, ushuru huo utahesabiwa kwa wastani wa thamani kwa mujibu wa ushahidi unaofaa ambao unaweza kupatikana kwa dhamana hiyo kwa tarehe ya hati hiyo.

(3) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, endapo makubaliano ya uhaulishaji au uhaulishaji wa mali ni hisa, au dhamana ya soko, au dhamana nyengine na kwa maoni ya Kamishna makubaliano hayajitoshelezi, kuhusiana na thamani ya hisa au dhamana iliyowekwa kama ilivyoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ushuru utatozwa kwa thamani ya mali iliyohaulishwa.

Uhaulishaji wa nyaraka za hisa.

**38.**-(1) Uhaulishaji wa hisa yoyote au hisa zozote au katika soko la hisa au fedha za shirika, kampuni au jumuiya yoyote kwa vyovyote ilivyo, hautasajiliwa au kuingizwa katika vitabu vya kumbukumbu vya shirika hilo, kampuni au jumuiya hiyo ndani

Zanzibar isipokuwa uhaulishaji huo umewekewa stempu sahihi na kila uhaulishaji utahifadhiwa katika afisi ya usajili wa shirika, kampuni au jumuiya hiyo kwa kipindi kisichopungua miezi kumi na mbili kutoka tarehe ya uhaulishaji huo.

(2) Mtu ambaye atashindwa kufuata masharti ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua Shilingi Milioni Mbili na isiyozidi Shilingi Milioni Tano.

(3) Uhaulishaji wa hisa kwa njia ya kubadilishana hisa au mali nyengine yoyote itakuwa kwa mujibu wa kiwango cha ushuru kwa asilimia kulingana na thamani kuhusiana na makubaliano ya uhaulishaji huo kama kwamba uhaulishaji huo ulifanywa kwa njia ya mauzo.

Uhaulishaji kwa njia ya mauzo.

**39.**-(1) Hati ambayo mali yoyote imehaulishwa kisheria au kwa haki au amepewa mtu mwengine kwa njia ya kubadilishana, itatathminiwa na kulipiwa ushuru ipasavyo.

(2) Katika masharti yote ya sheria hii yanayohusiana na uhaulishaji kwa njia ya mauzo, kila kumbukumbu inayohusiana na mauzo au manunuzi itachukuliwa ipasavyo kama ni mwendelezo wa kubadilishana.

Fedha zinazostahiki kulipwa.

**40.** Endapo fedha ambazo zinaweza kudaiwa au kulipwa kuhusiana na dhamana yoyote isiyokuwa dhamana ya soko itasawazishwa au imekubaliwa kusawazishwa, hati ambayo usawazishaji huo umefanywa au umekubaliwa kufanywa itatozwa kiwango cha ushuru kwa asilimia kwa mujibu wa fedha hizo, na kwa upande wa dhamana za soko itatozwa kwa kiwango cha ushuru kwa asilimia ya dhamana hiyo.

Ikiwa hati mbalimbali moja tu itatozwa.

**41.**-(1) Endapo hati mbalimbali zinazotekelezwa kwa kuwezesha usawazishaji wa mali hiyo na kiwango cha ushuru kinachotozwa kwa asilimia kulingana na usawazishaji huo kinazidi Shilingi Laki Moja, moja tu kati ya hati hizo itatozwa ushuru kwa kiwango cha asilimia.

(2) Usawazishaji uliofanywa kulingana na makubaliano yaliyopita au masharti ambayo usawazishaji wowote wa kiwango cha ushuru kwa asilimia kinazidi Shilingi Laki Moja kimelipwa kuhusiana na mali hiyo haitatozwa kiwango cha ushuru kwa asilimia cha usawazishaji.

(3) Katika kila jambo lililotajwa chini ya kifungu hiki, hati ambazo hazikutozwa ushuru kwa kiwango cha asilimia zitatozwa ushuru wa Shilingi Laki Moja.

Dhamana za hisa.

**42.** Dhamana za hisa, au hati yoyote kwa mtoaji iliyotolewa na au kwa niaba ya kampuni au jumuiya zilizoundwa au kuanzishwa Zanzibar na zikawa na hadhi kama dhamana ya hisa, au hati yoyote ya hisa kwa mtoaji, imetolewa bila ya kuwekwa

stempu sahihi, kampuni au jumuiya inayotoa hati hiyo itakuwa imetenda kosa na itatozwa faini isiyopungua Shilingi Milioni Mbili na isiyozidi Shilingi Milioni Tano.

Hundi zilizokuwa hazijawekwa stempu.

**43.**-(1) Kwa mujibu wa kifungu hiki, mtu yeyote anayetoa, anayepokea, anayethibitisha, anayehaulisha, anayepatana, anayewasilisha malipo au anayelipa hundi yoyote inayopaswa kutozwa ushuru na haikuwekwa stempu sahihi, ataadhibiwa chini ya Sheria hii.

(2) Mtu anaechukua au anayepokea kutoka kwa mtu mwengine yeyote hundi hiyo, iwe kwa malipo au dhamana au kwa manunuzi au vyenginevyo, hatakuwa na haki ya kurejeshewa au kuifanya itumike tena kwa madhumuni mengine yoyote.

(3) Itakapotokea hundi yoyote imepokewa au imewasilishwa bila ya kuwekwa stempu sahihi, mfanyakazi yeyote wa benki ambaye imewasilishwa kwake katika hatua za kawaida za kibiashara anaweza:

(a) kuweka stempu sahihi ambayo haikuwekwa kihalali; au

(b) Ikiwa hundi haina stempu,kuweka stempu au stempu zote mbili kwa kiwango cha ushuru ambacho hundi hiyo inastahiki kutozwa na kwa kiwango chochote kitakachohalalisha adhabu iliyoelezwa chini ya Sheria hii, na kuweka stempu kinyume na utaratibu kama kwamba alikuwa ni mtu aliyeidhinishwa; na hundi hiyo, kwa hali inayoashiria kutozwa ushuru, itachukuliwa kuwa ni halali na imepokelewa.

Mfanyakazi wa benki au hawala ya benki.

**44.** Kwa madhumuni ya sheria hii, mtu yeyote anayetekeleza shughuli za kibenki Zanzibar zenye uhusiano na benki na hawala za benki atajumuisha:

(a) hati ya kubadilishana au hawala ya fedha inayotolewa na benki kwa malipo ya fedha kwa mteja anapohitaji; na

(b) hati ya kubadilishana au hawala ya fedha iliyotolewa ambayo inaruhusu au inakusudia kumruhusu mteja au mmiliki, bila ya uthibitisho au bila ya uthibitisho mwengine wakati wa kutoa hati hizo, ama imeelezwa au haikuelezwa na katika namna yoyote ile, hati au hawala imetayarishwa au imetengenezwa kwa mtu mwengine yeyote.

Masharti ya kutoza ushuru wa risiti.

**45.**-(1) Mtu yeyote anayefanya shughuli ya biashara au taaluma Zanzibar ambaye anapokea pesa kwa kiwango cha Shilingi Elfu Moja au zaidi kwa makubaliano ya kupokea au kuuza bidhaa yoyote au huduma Zanzibar, atatoa risiti iliyowekwa stempu sahihi kwa kiwango kilichopokelewa, iwe imedaiwa au haikudaiwa.

(2) Ushuru kuhusiana na risiti unaweza kutambuliwa kwa stempu ya kubandikwa ambayo itafutwa na mtu ambaye amepewa risiti kabla hajaitoa kumpa mtu mwengine.

(3) Benki au mfanyakazi wa benki, au mtu anayelipwa aliyeandikwa katika hati au ruhusa, ama imeambatana na maneno ya kupokea au vyenginevyo katika hali ya kawaida ya kibiashara kama benki au mfanyakazi wa benki, au anayelipwa katika hati ya kubadilishana, hundi au hawala zilizowekwa stempu sahihi, kama imelipwa kwa ruhusa, haitakuwa risiti inayotozwa ushuru.

Utaratibu wa ushuru katika risiti.

**46.**-(1) Kamishna anaweza, kwa kuzingatia masharti ya kifungu hiki, kuingia katika makubaliano na mtu yeyote kwa utaratibu wa kutoza ushuru wa stempu katika kipengele cha "risiti", au kuruhusu kutolewa, au kuhusiana na malipo ya fedha katika Jadweli la Kwanza la Sheria hii kwa risiti iliyoruhusu kutolewa na au kwa niaba ya mtu huyo kama itakavyoweza kuainishwa katika makubaliano.

(2) Makubaliano yaliyofanywa, ikiwa kifungu hiki kitamtaka mtu aliyeingia makubaliano kuwasilisha kwa Kamishna kila kipindi kwa kuzingatia hati ambayo makubaliano hayo yanahusika, na kutoa taarifa kama Kamishna atakavyoeleza, na inaweza kujumuisha masharti na taratibu nyengine kama Kamishna atakavyoona inafaa.

(3) Endapo makubaliano yamefanywa chini ya kifungu hiki, hati yoyote ambayo makubaliano yanahusika na ambayo inashiria malipo hayo ya ushuru wa stempu kama Kamishna anavyoweza kuhitaji, haitatozwa ushuru wa stempu, lakini mtu ambaye makubaliano yamefanywa kwake atalipa kwa Kamishna, kwa kuweka katika akaunti yoyote ambayo imeelezwa katika makubaliano, fedha hizo, lakini kwa masharti ya kifungu hiki, zingeweza kutozwa kwa njia ya ushuru wa stempu kuhusiana na hati hizo zilizotolewa katika kipindi ambacho hesabu hizo zinahusika.

(4) Iwapo mtu anafanya makosa katika kuwasilisha malipo yoyote yanayoelezwa katika makubaliano yoyote yaliyofanywa chini ya kifungu hiki, au katika ulipaji wa ushuru unaotakiwa kulipwa katika akaunti hiyo, atakuwa ametenda kosa na masharti ya adhabu ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi yatatumika ipasavyo.

Ritani na malipo.

**47.**-(1) Mtu, taasisi au wakala aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 5 cha Sheria hii, atatakiwa kuwasilisha marejesho ya mwezi na kulipa katika utaratibu ulioelezwa na Kanuni za Sheria hii.

(2) Tarehe ya mwisho ya uwasilishaji wa ritani na malipo iliyoelezwa katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi, itatumika katika kuwasilisha ritani na malipo chini ya

kifungu hiki, isipokuwa Kamishna atakavyoelekeza vyenginevyo kwa madhumuni ya kulinda ushuru unaotakiwa kulipwa chini ya Sheria hii.

(3) Endapo mtu atashindwa kuwasilisha ritani na malipo atakuwa ametenda kosa na masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi kuhusiana na kushindwa kuwasilisha **ritani** na malipo ya kodi yatatumika sambamba katika masharti ya kifungu hiki.

Hati zitakazotozwa ushuru tofauti.

**48.**-(1) Kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, hati iliyotayarishwa kwa makubaliano ambayo inatakiwa kutozwa ushuru wa Stempu, na pia kwa makubaliano mengine au makubaliano yenye thamani, yatatozwa ushuru wa stempu tafauti na kwa kila moja, kama vile ni hati tafauti, kwa kuzingatia kila makubaliano.

(2) Endapo kuna hati zaidi ya moja imeandikwa katika waraka mmoja, kila moja kati ya hati hizo itawekwa na kutozwa ushuru wa stempu tafauti ambao unastahiki kutozwa.

(3) Bila ya kujali masharti ya kifungu cha 7 cha Sheria hii, hati iliyotayarishwa na ikiwa imo ndani ya vipengele viwili au zaidi katika Jadweli la Kwanza la Sheria hii, endapo ushuru unaotozwa chini vipengele hivyo ni tafauti, utatozwa kwa ushuru wenye kiwango kikubwa.

(4) Hati iliyotayarishwa kwa makubaliano yanayohusiana na utozaji wa ushuru kwa kiwango cha ushuru kwa asilimia, na pia kwa makubaliano mengine au ya thamani, itatozwa ushuru tafauti na kwa kila moja, kama kwamba ilikuwa ni hati tafauti kulingana na kila makubaliano.

(5) Endapo mali imewekewa mkataba wa kuuzwa kwa makubaliano ya aina moja, kwa mali yote iliyohaulishwa kwa mnunuzi katika maeneo tafauti kwa hati tafauti, makubaliano yatagaiwa katika namna ambayo wahusika watakavyoona inafaa kwamba mkataba pekee kwa kila sehemu au eneo tofauti, uhaulishaji unahusiana na hati hiyo na kwamba uhaulishaji huo utatozwa kiwango cha ushuru kwa asilimia kwa kuzingatia mkataba huo wa kipekee.

Kivuli au nakala.

**49.**-(1) Kivuli au nakala ya hati inayotozwa ushuru wa stempu haitawekwa stempu isipokuwa:

(a) itawekwa stempu kama hati halisi;

(b) itaonesha malipo ya ushuru wa stempu uliolipwa kwa mujibu wa hati halisi ambayo ni kivuli au nakala;

(c) itaonesha hati ya ushuru iliyotolewa kwa kivuli au nakala ya malipo ya ushuru wa stempu uliyolipwa kwa mujibu wa hati halisi ambayo ni kivuli au nakala; au

(d) itakuwa hati iliyothibitishwa na Kamishna kwamba ushuru wote na sahihi umelipwa kwa mujibu wa hati halisi ambayo ni kivuli au ni nakala.

(2) Kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki hakitatumika kwa nakala ya hati inayotozwa kama hati ya ukodishaji ambapo nakala ya hati haijakamilishwa na au kwa niaba ya mkodishaji au mtoaji.

Hati ambazo hazijawekwa stempu hazitotumika kama ushahidi.

**50.**-(1) Hati inayotozwa ushuru, isipokuwa hati iliyoekewa stempu sahihi:

(a) haitakubaliwa katika ushahidi kwa madhumuni ya mtu ambaye kwa Sheria au ridhaa ya wahusika wenye mamlaka kuchukuwa ushahidi; au

(b) haitafanyiwa kazi, haitasajiliwa au kuthibitishwa na mtu au afisa wa umma;

(2) Hati yoyote isiyokuwa hundi, au hati ya malipo, iliyowasilishwa kwa madhumuni ya kukubalika, imekubaliwa au inatakiwa kulipwa nje ya Zanzibar, au hawala, kwa kuzingatia misamaha yote, zitakubalika katika ushahidi zitakapolipiwa na malipo ya ushuru ambao hati inatozwa, au kwa hati ambayo imewekwa stempu isiyojitosheleza, kwa kiwango kinachotakiwa kulipwa ushuru pamoja na adhabu iliyoainishwa lakini:

(a) endapo mtu ambaye risiti iliyowekwa stempu, kutoka kwake inaweza kuhitajika na ametoa risiti isiyowekwa stempu, na risiti hiyo, kama itawekwa stempu itakubalika ni ushahidi dhidi yake, pia risiti itakubalika kuwa ni ushahidi dhidi yake kuhusiana na malipo ya adhabu iliyoainishwa kwa mtu aliyeitoa risiti hiyo;

(b) endapo mkataba au makubaliano ya aina yoyote yatafanywa kwa mawasiliano ya kimaandishi yanayojumuisha barua mbili au zaidi na barua yoyote miongoni mwa barua hizo itakuwa na stempu sahihi, mkataba au makubaliano yatachukuliwa yamewekewa stempu sahihi;

(3) Kifungu hiki hakitazuia kukubaliwa kwa hati katika mahkama yoyote ambapo hati imetolewa na au kwa niaba ya Serikali, au endapo itakuwa na hati halali iliyothibitishwa na Kamishna kama ilivyoelezwa na Sheria hii.

Kamishna kutoa maoni.

**51.**-(1) Kamishna anaweza kutakiwa na mtu kutoa maoni kutokana na hati iliyotolewa, kuhusu:

(a) iwapo hati inastahiki kulipiwa ushuru; na

(b) kiwango cha ushuru ambacho hati hiyo inastahiki kutozwa ushuru, iwapo unastahiki kulipwa.

(2) Kamishna anaweza kumtaka mtu ampatie maelezo ya hati na pia ushahidi muhimu kwa ajili ya kutoa maamuzi iwapo maelezo na mazingira yanayoathiri dhima ya hati kulipiwa ushuru, au kiwango cha ushuru kinachotozwa katika hati yamekamilika na yako sahihi.

(3) Endapo kwa maoni ya Kamishna kwamba hati haitozwi ushuru, hati hiyo inaweza kuwekewa stempu maalumu inayonesha kwamba hati hiyo haitozwi ushuru.

(4) Endapo kwa maoni ya Kamishna kwamba hati inapaswa kutozwa ushuru, ushuru utatathminiwa, na hati itawekewa stempu kwa mujibu wa tathmini.

Uwezo wa Kamishna kurejesha malipo ya adhabu au ushuru uliozidi kwa baadhi ya mazingira.

**52.**-(1) Mtu anaweza kuomba kwa Kamishna kurejeshewa malipo ambayo yalilipwa kimakosa ya ushuru wa stempu au ushuru wa stempu uliolipwa zaidi ya ushuru uliopaswa kulipwa kuhusiana na hati.

(2) Mtu anaweza kudai kurejeshewa ushuru uliolipwa kimakosa kuhusiana na hati ambayo haikupaswa kulipiwa ndani ya mwaka mmoja baada ya tarehe ya ushuru huo kulipwa.

(3) Maombi kuhusiana na marejesho chini ya kifungu hiki yatawasilishwa kwa Kamishna ndani ya miezi mitatu kuanzia tarehe ya malipo ya ushuru wa stempu.

(4) Endapo, kwa maoni ya Kamishna, ushuru wa stempu wa ziada ambao ulipaswa kutozwa kisheria umetozwa na kulipwa, Kamishna anaweza:

(a) kutumia kilichozidi kwa kupunguza kodi nyengine kutoka kwa mtu huyo;

(b) kutumia kilichobakia katika ziada, kama kipo, katika kupunguza deni la mtu analopaswa kulipa kodi nyengine yoyote ambayo haibishaniwi; na

(c) kurejesha kilichobakia, kama kipo, kwa mtu huyo.

(5) Kamishna, ndani ya siku thelathini za kufanya maamuzi chini ya kifungu hiki, atampatia mtu anayeomba marejesho, taarifa ya maandishi kuhusiana na maamuzi hayo.

(6) Mtu ambaye hakuridhika na maamuzi ya Kamishna chini ya kifungu hiki, anaweza kukata rufaa dhidi ya maamuzi kwa mujibu wa utaratibu wa pingamizi na rufaa uliowekwa katika Sheria inayohusiana na rufaa za kodi.

Tathmini ya ushuru kwa mazingira maalumu.

**53.**-(1) Endapo hati inatozwa kiwango cha ushuru kwa asilimia kuhusiana na fedha yoyote iliyotajwa kwa fedha isiyokuwa ya kitanzania, ushuru utahesabiwa kwa thamani ya fedha za kitanzania.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kiwango cha kubadilishia fedha kitakachotumika kitakuwa ni kiwango cha kuuza na kununua kitakachotolewa na Benki Kuu ya Tanzania.

(3) Endapo hati inajumuisha maelezo ya viwango vya sasa vya kubadilishia fedha au wastani wa bei na kuwekwa stempu kwa mujibu wa maelezo hayo, kuhusiana na maelezo, itachukuliwa kuwa imewekewa stempu sahihi, isipokuwa hadi ikionesha kwamba si sahihi na kwamba kiuhalisia hati haikuwekwa stempu sahihi.

(4) Endapo hati inayopaswa kutozwa ushuru kwa kiwango cha ushuru kwa asilimia, ushuru huo kuhusiana na kile kilichomo ndani ya hati kama kilivyo wakati wa kutolewa, kwa tathmini:

(a) iwapo kiwango maalum kimeelezwa katika hati, kitahesabiwa kwa kiwango hicho; au

(b) iwapo kiwango maalumu hakikuelezwa katika hati, na:

(i) kiwango cha juu, au kiwango kisichofahamika au vyenginevyo, kimeelezwa katika hati, ama au kwa kiwango kisichokuwa cha chini, kiwango kisichofahamika au vyenginevyo, kitahesabiwa kiwango hicho cha juu; au

(ii) hakuna kiwango cha juu, kiwango kisichofahamika au vyenginevyo katika hati lakini kiwango cha chini, kisichofahamika au vyenginevyo, kitahesabiwa kiwango hicho maalumu.

(c) endapo kiwango maalumu kimeelezwa katika hati na hati inajumuisha maelezo ya kiwango cha ziada, kiwango kisichofahamika au

vyenginevyo ambacho hakikuelezewa katika hati, kitahesabiwa kwa kiwango cha jumla cha fedha kwa kiwango hicho maalumu.

Muda wa kuweka stempu nyaraka.

**54.**-(1) Kila hati inayopaswa kutozwa ushuru ambayo imetolewa Zanzibar, isipokuwa kama imeelezwa vyenginevyo katika sheria hii, itawekewa stempu iliyo sahihi ndani ya siku thelathini za utolewaji wake, ikiwa hati inatolewa na watu wawili au zaidi kipindi hicho cha siku thelathini kitahesabiwa kuanzia tarehe ambayo hati imewekwa saini na mtu anayefuatia au watu wa mwisho.

(2) Isipokuwa kama imeelezwa vyenginevyo katika Sheria hii, hati inayopaswa kutozwa ushuru imetolewa nje ya Zanzibar itawekewa stempu sahihi ndani ya siku thelathini baada ya tarehe ambayo imepokelewa kwa mara ya kwanza ndani ya Zanzibar na mtu anaepokea kwa mara ya kwanza hati yoyote ya aina hiyo ataandika juu ya hati hiyo tarehe ya kupokea na sahihi.

(3) Ikiwa mtu anapaswa kuweka stempu hati yoyote na yupo katika mashaka kama anapaswa kuweka stempu au ana wajibu wa dhima hiyo, ndani ya siku ishirini baada ya kutolewa hati hiyo atakuwa ameiwasilisha hati hiyo kwa afisa aliyeidhinishwa kwa ajili ya kuiwasilisha kwa Kamishna ili kutoa maamuzi kuwa dhima hiyo inaendelea au ana wajibu wa dhima hiyo, kwa madhumuni ya kifungu hiki, tarehe ya kutolewa hati hiyo itachukuliwa kuwa tarehe ambayo uamuzi wa Kamishna umetolewa kwa mtu ambaye ameiwasilisha hati hiyo kama ilivyoainishwa.

(4) Hati yoyote iliyotolewa nje ya Zanzibar na inakusudiwa kutumika kuhaulisha mali yoyote isiyohamishika au mali yoyote inayohamishika, isipokuwa mali zilizowekewa dhamana zilizotolewa na, au hisa, katika kampuni ikiwa mali hiyo imekusudiwa kuhaulishwa ipo katika eneo lolote la Zanzibar, itatozwa ushuru wa stempu kwa mujibu wa Jadweli la Kwanza.

Ruhusa kwa stempu zilizoharibika.

**55.**-(1) Kamishna anaweza, kupitia maombi kwa namna ilivyoelezwa katika kanuni zozote zilizotungwa chini ya Sheria hii, kutoa ruhusa ya stempu zilizotolewa kimakosa na zimeharibika, au haziwezi kutumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa kwa kubadilisha stempu nyengine kwa thamani sawa au kumpa mmiliki kiwango sawa kwa ruhusa ya Hazina.

(2) Kwa namna yoyote ambayo ruhusa imetolewa kwa stempu zilizoharibika au zilizotumika vibaya, Kamishna au afisa aliyeidhinishwa anaweza kutoa mbadala wake:

(a) stempu nyengine zenye maelezo na thamani sawa;

(b) ikiwa itahitajika na akiona inafaa, stempu nyengine yenye kiwango sawa katika thamani; au

(c) kimakosa imetumika stempu yoyote kwa hati ambayo haitozwi ushuru wowote;

(d) stempu yoyote iliyotumika kwa hati iliyotumika kimakosa na kwamba hazifai kutumika chini ya Sheria hii;

(e) kwa uwezo alionao, kwa kiwango sawa na thamani ya fedha, kupunguza shilingi moja au sehemu ya shilingi kwa kila Shilingi Elfu Moja.

Mazingira ya stempu zilizoharibika.

**56.** Kamishna anaweza kutoa ruhusa kwa ajili ya stempu zilizoharibika kwa mazingira yafuatayo:

(a) stempu ya waraka wowote iliyowekwa kimakosa na baada ya kutiwa sahihi imeharibika, imeondoshwa au ina makosa ya kiuandishi au njia nyengine na kuifanya isiweze kutumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa kabla hati hiyo kuandikwa kwenye waraka unaotolewa na mtu mwengine;

(b) stempu ya waraka ambayo imeandikwa yote au sehemu, lakini haikusainiwa au haikukamilishwa na mtu mwenye waraka huo;

(c) kwa mazingira ya hati za malipo, hundi au hawala:

(i) stempu iliyopo katika hati ya malipo au hundi iliyosainiwa na au kwa niaba ya mtoaji ambayo haikukubaliwa au kutumiwa kwa namna au imetolewa kupitia mikono ya mtoaji kwa madhumuni mengine kwa njia ya kuiwasilisha kwa ajili ya kukubalika, ikiwa waraka ambao stempu imewekwa hauoneshi sahihi iliyokusudiwa kama au kwa kukubaliwa kwa hati ya malipo au hundi zitakazoandikwa au kutolewa baadae;

(ii) stempu iliyopo katika hawala iliyosainiwa na au kwa niaba ya aliyeitayarisha na ambayo haijatumika kwa namna yoyote au imetolewa kupitia mikono ya mtayarishaji;

(iii) stempu iliyotumika au kukusudiwa kutumika kwa ajili ya hati za malipo, hundi au hawala kwa au, kwa niaba ya mtoaji, lakini ambayo kwa kitendo chochote cha uondoshaji au kimakosa imeharibiwa au imefanywa kuwa haiwezi kutumika,

ingawaje katika mazingira ya hati za malipo au hundi, inaweza kuwasilishwa kwa ajili ya kukubaliwa au kuthibitishwa, au ni hawala inaweza kuwasilishwa kwa anayelipwa, ikiwa hati nyengine ya malipo imekamilishwa na imewekwa stempu sahihi, hundi au hawala imetolewa inafanana kwa kila maelezo, isipokuwa katika kurekebisha makosa, kwa hati za malipo zilizoharibika, hundi au hawala;

(d) stempu iliyotumika kwa hati iliyotolewa na mtu anayehusika na hati hiyo, ambayo:

(i) itagundulika kuwa si halali;

(ii) itagundulika kuwa haifai kwa sababu ina makosa ndani yake, au kwa madhumuni halisi iliyokusudiwa;

(iii) kwa sababu ya kifo cha mtu ambae hati hiyo ilikuwa ni muhimu kutolewa na haikutolewa, au alikataa kuitoa, haiwezi kukamilishwa kwa ajili kuwezesha makubaliano yaliyokusudiwa katika namna iliyopendekezwa;

(iv) kwa ukamilishaji wake kwa sehemu kubwa, na hawezi au anakataa kutia saini, haijakamilika na haijitoshelezi kwa madhumuni ambayo hati hiyo ilikusudiwa;

(v) kwa sababu ya mtu kukataa kutekeleza wajibu uliomo ndani ya hati, au kutoa fedha zozote za awali zilizokusudiwa kwa ajili kuhakikishia malipo, au kwa kukataa au haijatolewa na afisi yoyote, kwa ujumla ameshindwa kwa madhumuni yaliyokusudiwa;

(vi) itakuwa haifai kutumika kwa muamala uliokusudiwa kufanyika na ukafanywa na hati nyengine baina ya watu hao wanaohusika na ikaonesha stempu isiyopungua thamani yake;

(vii) ina mapungufu katika thamani na muamala uliokusudiwa kufanyika na ukafanywa na hati nyengine baina ya watu hao wanaohusika na ikaonesha stempu isiyopungua thamani yake; au

(viii) imekosewa na imesainiwa kimakosa, na badala yake ambapo hati nyengine imetayarishwa baina ya watu hao wanaouhusika na kwa madhumuni sawa iliyotolewa na kuwekwa stempu sahihi, ikiwa hati imetolewa na hakuna shauri lolote lilofunguliwa

ambapo hati ingeweza kutolewa kama ni ushahidi na kama hati itatolewa itafutwa.

Ruhusa katika kubadilisha stempu.

**57.** Kamishna anaweza kuruhusu stempu zilizotayarishwa au kusambazwa kwa wakala chini ya Sheria hii, ikiwa kutakuwa na sababu zinazojitosheleza, stempu zilizozuiwa na kuhitajika na Serikali bila ya kujali kwamba ushuru kuhusiana na waraka zilizowekwa stempu zimelipiwa ipasavyo.

Tathmini ya Mtathmini wa Serikali.

**58.** Wakala aliyeidhinishwa atawasilisha kwa Mtathmini Mkuu wa Serikali uhaulishaji wowote wa mauzo ya mali isiyohamishika kabla au baada ya usajili wa hati husika kwa ajili ya kuweka thamani halisi ya soko kwa mali hiyo, tarehe ambayo uhaulishaji umefanyika kwa madhumuni ya kuainisha ushuru sahihi.

Kumbukumbu za kieletroniki.

**59.**-(1) Endapo hati ambayo inapaswa kutozwa ushuru chini ya Sheria hii, ikiwa ipo katika mfumo wa kumbukumbu za kieletroniki, nakala iliyochapwa ya hati hiyo itatayarishwa na kuwekewa stempu kwa namna zote kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hati ambayo ipo katika mfumo wa kumbukumbu za kielektoroniki haitawekewa stempu hadi nakala iliyochapishwa ya hati hiyo imewekewa stempu sahihi.

## SEHEMU YA NNE
## USHURU WA STEMPU KATIKA UENDESHAJI WA BIASHARA

Viwango vya kutoza.

**60.**-(1) Viwango vya kutoza kwa bidhaa na huduma chini ya Sheria hii vitawekwa kama ifuatavyo:

(a) mfumo wa malipo ya mkupuo bidhaa na huduma zinazotozwa kodi utakaofanywa kwa msingi wa robo mwaka ambapo mlipakodi atatozwa kwa kiwango maalum kilichoainishwa katika Jadweli la Pili la Sheria hii.

(b) mfumo wa malipo kwa mujibu wa mauzo ambao utajumuisha walipakodi wote wanaotozwa kiwango cha ushuru kwa asilimia kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Nne la Sheria hii ambao utazingatia:

(i) asilimia 3 ya thamani ya bidhaa na huduma,

(ii) asilimia 2 ya thamani ya bidhaa na huduma zilizoingizwa ambazo zimesamehewa chini ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani.

(2) Waziri anaweza, kwa amri iliyotangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali, kurekebisha, kubadilisha au kuweka upya Jadweli kama ifuatavyo:

(a) kubadilisha msingi wa tozo katika mfumo wa malipo ya mkupuo na viwango vilivyoainishwa katika Jadweli la Pili na Jadweli la Tatu;

(b) kuongeza au kupunguza kiwango chochote cha ushuru kilichoainishwa katika Jadweli la Kwanza; au

(c) kuongeza, kupunguza na kurekebisha huduma au bidhaa au aina ya huduma au bidhaa na viwango vilivyoainishwa katika Jadweli la Pili, Tatu na la Nne la Sheria hii.

Shughuli zinazotozwa kodi.

**61.** Kwa madhumuni ya masharti ya kifungu hiki, shughuli inayotozwa kodi maana yake ni shughuli inayofanywa na mtu, ama kwa faida au bila ya faida, ikiwa shughuli hiyo itajumuisha au inakusudia kujumuisha usambazaji wa huduma au bidhaa kwa mtu mwengine na inajumuisha biashara, uzalishaji, matukio yenye maumbile ya kibiashara ambayo hayatajumuisha:

(a) shughuli za muajiriwa anayetoa huduma kwa ajili ya muajiri;

(b) shughuli zinazofanywa na mkurugenzi au mtu mwengine yeyote katika kampuni isipokuwa endapo, katika kufanya biashara, mtu anakubali ofisi na kutoa huduma kama msimamizi wa ofisi hiyo, ambapo kwa namna hiyo huduma hizo zitajulikana kuwa zimefanywa katika biashara au kuendeleza biashara; na

(c) shughuli zinazofanywa na taasisi za Serikali Kuu au Serikali za Mitaa au Mabaraza ya Miji, isipokuwa kwa kiasi kwamba shughuli hizo ni moja ambazo taasisi inazifanya kikawaida na mtu mwengine kwa ajili ya faida.

Thamani inayotozwa kodi.

**62.**-(1) Thamani inayotozwa kodi kwa usambazaji wa bidhaa na huduma itazingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi na yatatumika kama yalivyo kwa thamani iliyotozwa kodi chini ya Sheria hii.

(2) Ushuru wa stempu kwa bidhaa zinazoingizwa nchini na kusamehewa kodi chini ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani zitatozwa ushuru kwa kiwango kilichoelezwa katika kifungu cha 3 (3) (a) cha Sheria hii.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi, thamani ya utozaji wa kodi kwa bidhaa zinazoingizwa Zanzibar na kusamehewa kodi, kwa madhumuni ya Sheria hii itakuwa kwa kiwango cha jumla cha:

(a) thamani ya uingizaji huo kwa madhumuni ya ushuru wa forodha;

(b) kiwango cha ushuru wa forodha kinacholipwa.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Waziri anaweza, baada ya kuzingatia maslahi ya umma, kwa amri itakayotangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali, kuainisha bidhaa au huduma maalum ambazo zitatozwa kiwango cha ushuru wa stempu kisichokuwa kiwango kilichoelezwa katika kifungu cha 3(3)(a).

Utambulisho wa walipakodi.

**63.**-(1) Kwa madhumuni ya kuwatambua walipakodi chini ya Sheria hii, Kamishna, kwa taarifa itakayotangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali, ataamua na kutambua maeneo katika mikoa tofauti.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Kamishna atakuwa na uwezo wa kuwapanga walipakodi katika maeneo yaliyotambuliwa kwa madhumuni ya kulipa ushuru wa stempu.

(3) Kamishna anaweza kumtaarifu mlipakodi aliyetambuliwa katika eneo lililotambuliwa, kiwango kinachotakiwa kulipwa na tarehe za kufanya malipo.

Udhibiti, tathmini, na ukusanyaji.

**64.**-(1) Kamishna atawajibika kudhibiti, kutathmini, na kukusanya ushuru wa stempu.

(2) Kamishna atakuwa na uwezo wa kusimamia mambo yote yanayohusiana na ushuru wa stempu, na katika kusimamia uwezo huo anaweza kumteua mtu yeyote mwenye sifa ya kutekeleza uwezo na kazi zake chini ya Sheria hii au Kanuni.

(3) Kamishna anaweza, kwa masharti na makubaliano, kumteua mtu mwengine kama atakavyoona, kutekeleza kazi zozote za Kamishna chini ya Sheria hii, au kuhitaji uelewa wa kitaalamu au ujuzi kwa mujibu wa mipaka anayoona Kamishna inafaa.

(4) Mtu aliyeteuliwa chini ya kifungu hiki atatekeleza na kuhakikisha anawajibika kufuata masharti ya Sheria hii na Kanuni na atafanya yote yanayohitajika kuhusiana na hayo.

(5) Mtu aliyeteuliwa chini kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki itakapohitajika atawasilisha nyaraka zinazoainisha utambulisho wake kama itakavyoidhinishwa na Kamishna.

Kutambuliwa malipo ya ushuru wa stempu.

**65.**-(1) Mfumo wa malipo ya mkupuo utaelezwa katika Jadweli la Pili na la Tatu ya Sheria hii utazingatia yafuatayo:

(a) biashara maalum au usambazaji wa bidhaa na huduma ya mlipa kodi; yatalipwa kwa kila mwaka; na

(b) mauzo maalum ya mlipakodi; yatalipwa kwa kila robo mwaka;

(2) Mauzo maalum ya mlipakodi chini ya aya (a) ya kifungu kidogo cha (1) yatatolewa na stika au nyaraka nyengine yoyote kwa kila mwaka, kama risiti ya malipo ya ushuru na stika hizo au nyaraka zitamaliza muda ifikapo tarehe 31 Disemba ya kila mwaka.

Ritani na maelezo yake.

**66.** Mlipakodi chini ya malipo ya mkupuo wakati wa kuwasilisha malipo atalazimika kujaza fomu kama ya ritani kwa malipo yatakayofanywa kama ilivyoelezwa na Kamishna katika Kanuni.

Ukadiriaji wa thamani.

**67.**-(1) Kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 19 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Kamishna atafanya tathmini ya malipo ya mkupuo ya mlipakodi kwa mwaka chini ya Sheria hii, katika taarifa iliyoainishwa, iliyoelezwa na Kamishna katika Kanuni.

(2) Ikiwa mlipakodi ameshindwa kujaza fomu inayohitajika au kuwasilisha taarifa kwa Kamishna au hana taarifa kamili katika biashara yake, Kamishna atamfanyia tathmini ya mauzo ya mwaka mlipakodi huyo, kwa kutumia maamuzi sahihi.

## SEHEMU YA TANO
## MENGINEYO

Kushindwa kuonesha maelezo kamili kuhusiana na hati.

**68.** Mtu anayekusudia kudanganya, akatumia hati bila ya kutoa maelezo kamili na ya ukweli na mazingira yaliyoelezwa katika Sheria hii; au ameajiriwa au anahusika na au katika utayarishaji wa hati, anadharau au anaacha kutoa maelezo kamili au ukweli na mazingira, atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua Shilingi Laki Moja na isiyozidi Shilingi Laki Tano.

Usajili wa hati zisizowekewa stempu sahihi.

**69.** Mtu aliyesajili taarifa za hati zinazotozwa ushuru lakini hazijawekewa stempu sahihi kwa madhumuni ya kumbukumbu rasmi chini ya Sheria, atakuwa ametenda kosa na anastahiki kulipa faini isiyopungua Shilingi Laki Mbili na isiyozidi Shilingi Laki Tano.

Kuweka kikwazo katika usimamizi wa Sheria hii.

**70.**-(1) Endapo afisa wa umma ameidhinishwa na Kamishna kukusanya ushuru wa Stempu, bila ya dharura ya msingi anashindwa kutekeleza wajibu au amekiuka maadili atakuwa ni mkosa na masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma yatatumika.

(2) Endapo wakala mwengine yeyote aliyeidhinishwa na Kamishna kukusanya ushuru wa stempu bila ya dharura ya msingi anashindwa kutekeleza wajibu au anakataa kumruhusu mtu aliyeidhinishwa na Kamishna kufanya ukaguzi chini ya Sheria hii, atakuwa ametenda kosa na atawajibika kulipa faini isiyopungua Shilingi Laki Mbili na isiozidi Shilingi Laki Tano.

Makosa yanayohusiana na kuweka stempu katika hati, kuharibu na ukwepaji ushuru.

**71.** Mtu ambaye:

(a) kuhusiana na kuweka stempu katika hati yoyote au kuharibu stempu yoyote katika hati, kuitumia, kuingiza au kuithibitisha kwa tarehe isiyo sahihi; au

(b) atatoa maelezo yasiyo sahihi au mazingira yanayohusiana na maelezo ya hati, au ushuru ambao unapaswa kutozwa katika hati hiyo; au

(c) kwa kitendo cha makusudi au cha kukataa kufanya au kukwepa au kujaribu kusaidia mtu mwengine kukwepa ushuru wowote unaotozwa chini ya Sheria hii,

atakuwa ametenda kosa na atawajibika kulipa faini isiyopungua Shilingi Laki Tatu na isiyozidi Shilingi Laki Tano.

Kumiliki hati mbazo zimewekwa stempu kinyume na sheria.

**72.**-(1) Mtu anayefanya, anayesababisha kufanya au kwa kujua anasaidia, au anatoa msaada kwa mtu mwengine yeyote katika kufanya matendo yoyote kati ya yafuatayo:

(a) Kughushi stempu;

(b) Kuchapisha au kuweka stempu katika hati yoyote kwa stempu iliyoghushiwa akijua kwamba imeghushiwa;

(c) kwa nia ya kudanganya, kuchapisha au kuweka maelezo katika hati kutoka katika stempu iliyo halali.

(d) Kukata, kufunga au kwa njia yoyote ile kuondoa stempu katika hati yoyote, kwa lengo la kuhakikisha udanganyifu unafanywa katika stempu hiyo au kwa sehemu yoyote ndani yake;

(e) kuharibiwa kwa stempu yoyote, kwa nia ya kuitumia kiudanganyifu ;

(f) kwa nia ya kughushi, kuweka maelezo yoyote katika stempu au sehemu ya stempu ambayo, ama kwa lengo hilo au vyenginevyo, imekatwa, haitambuliki au kwa njia nyengine yoyote imeondoshwa kutoka katika hati yoyote;

(g) kufuta au kuondoa, au kufanya kitendo chochote kinachopelekea kufuta au kuondosha katika hati yoyote iliyowekwa stempu jina, kiasi, tarehe au jambo au kitu chochote kilichoandikwa kwa nia ya kufanya udanganyifu wowote utatumika katika hati,

(h) kuuza au kutangaza kuuza, au kueleza au kutumia, stempu zilizoghushiwa ambazo zimechapishwa kwa njia ya kughushi au kuweka katika stempu halisi, kwa kujua hati hiyo imeghushiwa au imechapishwa au imewekwa stempu;

(i) kwa kujua na bila ya sababu ya msingi, uthibitisho utakuwa juu yake, anayo stempu iliyoghushiwa au stempu yoyote ambayo ilichapishwa kwa njia ya kughushi au imetolewa katika hati halisi au katika stempu yoyote au sehemu ya stempu ambayo imekatwa kwa kughushiwa, imechanwa au imeondoshwa vyenginevyo katika hati yoyote au stempu ambayo imeghushiwa au hati yoyote iliyowekwa stempu iliyoondolewa jina, kiwango, tarehe au jambo jengine au kitu kilichofutwa kwa udanganyifu au vyenginevyo, aidha imeondoshwa kwa uhalisia au muonekano;

(j) kwa nia ya kughushi na kwamba stempu inaweza kutumika kwa mara nyengine, kuondosha au kusababisha kuondoshwa stempu ya wazi katika hati yoyote;

(k) kuuza au kutangaza kuuza au kuelezea stempu yoyote ya kubandikwa ambayo kwa uelewa wake, imeondoshwa, au imeelezea hati yoyote ambayo inayo stempu yoyote ya wazi ambayo kwa uelewa wake imeondoshwa kama ilivyoelezwa,

atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua Shilingi Laki Tatu na isiyozidi Shilingi Milioni Moja au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja faini na kifungo.

(2) Mtu ambae bila ya mamlaka ya kisheria au sababu ya msingi, uthibisho utakuwa ni juu yake, amenunua au kupokea au kwa kujua anayo au amehifadhi:

(a) waraka wowote uliotayarishwa au kutolewa kwa lengo la kuweka stempu na au kwa mamlaka husika kabla ya waraka huo kuwekewa stempu sahihi na au kutolewa kwa matumizi ya umma; au

(b) zana yoyote, stempu, mashine ya kurudufu, au kitu chengine pekee kinachotumika katika kutengeneza waraka huo;

atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini ya Shilingi Laki Tano au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili au vyote faini na kifungo.

Stempu zilizoghushiwa.

**73.** Mtu yeyote aliyeidhinishwa kuuza au kusambaza stempu, akiwa amekutwa na stempu iliyoghushiwa, hadi itakapothibitika vyenginevyo, itachukuliwa kuwa amekutwa na stempu, akijua kuwa imeghushiwa na amekusudia kuuza, kutumia au kuisambaza, atakuwa ametenda kosa na atatozwa faini isiyopungua Shilingi Laki Tano na isiyozidi Shilingi Milioni Moja.

Adhabu za Jumla.

**74.** Mtu ambaye anakwenda kinyume na sharti la Sheria hii, ambalo hakuna adhabu iliyoelezwa, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua Shilingi Laki Moja na isiyozidi Shilingi Laki Tano au kifungo kwa muda usiopungua mwezi mmoja na usiozidi miezi mitatu.

Uwezo wa kuchunguza.

**75.**-(1) Mtu ambae amekutwa nazo au zipo katika umiliki wake, mashine ya kurudufu, vitabu, taarifa, daftari la usajili, waraka au fomu nyengine za kumbukumbu na ukaguzi umefanywa kulinda ulipaji wa ushuru chini ya Sheria hii, au kuthibitisha au kugundua udanganyifu au ukiukwaji wowote kuhusiana na ushuru huo, kwa muda unaokubalika, bila kujali chochote chengine kinachopingana na sheria nyengine, atatakiwa kumruhusu mtu yeyote aliyeidhinishwa na Kamishna kukagua nyaraka hizo na kuchukua taarifa, nakala au sehemu ya nyaraka hizo kama atakavyoona inafaa bila ya ada au zawadi.

(2) Mtu ambaye anakataa kuruhusu au kuzuia ukaguzi huo au uchukuaji wa taarifa, nakala au sehemu ya taarifa atakuwa ametenda kosa na atatozwa faini isiyopungua Shilingi Laki Mbili na isiyozidi Shilingi Laki Tano.

Uwezo wa kupata taarifa.

**76.**-(1) Afisa aliyeidhinishwa, kama atakavyoona inafaa katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii, atakuwa na uwezo kamili wa kuingia katika maeneo yote, majengo na pahala popote, na kukagua vitabu vyote na kumbukumbu, ama zipo katika dhamana au umiliki wa afisa wa umma au taasisi inayojitegemea au mtu mwengine yeyote, kwa madhumuni ya kuthibitisha thamani ya soko kwa mali yoyote au kuthibitisha maelezo yoyote au kukagua vitabu vyovyote au kumbukumbu ambazo afisa aliyeidhinishwa ataona inafaa au zinahusika moja kwa moja kwa madhumuni ya Sheria hii, au anazingatia utoaji wa taarifa yoyote inayohitajika kwa madhumuni ya Sheria hii na anaweza bila ya ada au zawadi, atachukua sehemu ya taarifa au nakala za vitabu hivyo au nyaraka.

(2) Afisa aliyeidhinishwa anaweza kuwa navyo vitabu hivyo au nyaraka endapo kwa maoni yake:

(a) Ukaguzi au utoaji nakala au uchukuaji wa taarifa hauwezi kutekelezeka bila ya kuchukuliwa;

(b) Vitabu au nyaraka vinaweza, kuzuiwa, kufichwa au kuharibiwa isipokuwa vitakapochukuliwa;

(c) Vitabu au nyaraka zinaweza kuhitajika kama ushahidi katika shauri lililofunguliwa au kuanzishwa kwa madhumuni yoyote ya Sheria hii.

(3) Mtu ambaye amemzuia au kumuekea vikwazo afisa aliyeidhinishwa au mtathmini yoyote aliyeidhishwa na afisa aliyeidhinishwa, katika utekelezaji wa mamlaka yake chini ya kifungu hiki, au mtu ambaye amekataa au ameshindwa kufuata masharti chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki au kwa maelekezo yoyote yaliyotolewa kwa nia njema na Kamishna au mtathmini kwa madhumuni yoyote ya kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa na atatozwa faini isiyopungua Shilingi laki Tano na isiyozidi Shilingi Milioni Moja.

Uwezo wa kusamehe malipo ya ushuru katika hati.

**77.**-(1) Kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa chini ya Kanuni za Sheria hii, ushuru wowote ambao unatozwa kuhusiana na uhaulishaji wa hati au aina ya hati chini ya Sheria hii unaweza kupunguzwa au kusamehewa na Waziri kwa sababu ya msingi ya maslahi ya umma.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ushuru hautatozwa katika nyaraka zifuatazo:

(a) hati yoyote iliyotolewa na au kwa niaba au kwa maslahi ya Serikali ambapo ushuru ungepaswa kulipwa na Serikali.

(b) hati yoyote inayopaswa kutozwa ushuru ambayo imesamehewa kutokana na malipo chini ya mkataba au makubaliano ya nchi zilizoainishwa ambazo Serikali ni sehemu ya makubaliano hayo.

(3) Kampuni yoyote ambayo imeidhinishwa chini ya Sheria ya Ukuzaji wa Vitega Uchumi Zanzibar haitahitajika kulipa ushuru iwapo msamaha utatolewa chini ya Sheria hii.

Kanuni.

**78.**-(1) Waziri anaweza, kila baada ya muda, kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa Sheria hii; na kuweka:

(a) mambo yaliyoelezwa katika masharti ya Sheria hii; na

(b) namna ambayo thamani ya hati itatumika kwa ajili ya malipo ya ushuru,

(2) Waziri anaweza, kwa amri iliyochapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali kurekebisha, kuongeza au kuweka upya vipengele na viwango vilivyoelezwa katika Jadweli za Sheria hii.

(3) Waziri anaweza kutunga kanuni zinazohusiana na mfumo na nyaraka za kuwasilishwa katika maombi ya usajili, na taarifa zitakazowekwa na walipakodi chini ya Sheria hii.

Kufuta na kubakiza.

**79.**-(1) Sheria ya Ushuru wa Stempu Nam. 6 ya mwaka 1996 inafutwa.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Kanuni ambazo zimetungwa chini ya Sheria ya Ushuru wa Stempu Nam. 6 ya mwaka 1996 zitaendelea kutumika hadi zitakapofutwa na Kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii.

(3) Jambo lolote lililofanywa chini ya Sheria iliyofutwa, litachukuliwa kama limefanywa chini ya Sheria hii.

## JADWELI LA KWANZA

**(Chini ya kifungu cha (6))**

## ORODHA YA HATI NA MALIPO

| Nam. | AINA YA HATI | USHURU WA STEMPU | MTU ANAEPASWA KULIPA |
|---|---|---|---|
| 1. | Uthibitisho wa Deni | 5,000/= | Mtu wa mwanzo aliyeitoa |
| 2. | Uthibitisho wa risiti kwa kiwango cha fedha au mali nyengine kwa kiwango cha thamani inayozidi Shilingi Elfu Hamsini. | 5,000/= | Mtu wa mwanzo aliyeitoa |
| 3. | Hati ya kuhalalisha umiliki. | 5000 /= | Mtu wa mwanzo aliyeitoa |
| 4. | Viapo ikiwemo viapo au tamko. | 5000 /= | Anaeapishwa |
| 5. | Makubaliano. | 0.5% | Mtu wa mwanzo aliyeitoa |
| 6. | Makubaliano kuhusiana na umiliki wa Hati ya matumizi ya ardhi, ahadi- ya jumla ya thamani. | 0.05% | Mtu wa mwanzo aliyeitoa |
| 7. | Uteuzi katika kutekeleza mamlaka, ikiwa wadhamini au mali. | 5000/= | Aliyeteuliwa – Mtu anaefanya au kutekeleza uwakala. |
| 8. | Tathmini inayofanywa isiyokuwa amri ya mahkama. | Hapana | Hapana |
| 9. | Hati ya kuanzisha Kampuni. | 20,000/= | Mteuzi |
| 10. | Kuweka saini aidha kwa mkono au muhuri. | 5,000/= | Anaetoa wasia |
| 11. | Zawadi kwa msuluhishi au muamuzi | 5,000/= | Mtu anaepokea zawadi. |
| 12. | Hati nyengine zozote ambazo hazijaelezwa kwa uwazi. | 5,000/= | Mtoaji hati |
| 13. | Hati ya malipo ambayo sio dhamana, hawala ya benki au hawala ya fedha. | 5,000/= | Anaepokea |
| 14. | Hawala ya fedha. | 10.000/= | Anaepokea au aliyekubali. |

| Nam. | AINA YA HATI | USHURU WA STEMPU | MTU ANAEPASWA KULIPA |
|---|---|---|---|
| 15. | Hati ya usafirishaji wa mizigo (ikiwemo kwa njia ya nchi kavu, angani na njia ya mawasiliano ya posta). | 5,000/= | Mtu ambae anesimamia mzigo (Nahodha/ Wakala) |
| 16. | Hati ya Mauzo - thamani yake | 0.5% lakini isizidi 100,000/= | aliyeidhinisha. |
| 17. | Dhamana (isiyokuwa dhamana ya mkopo wa benki) | 5,000/= | Mtu aliyestahiki kuweka stempu hati ya awali |
| 18. | Kubatilisha hati | 5,000/= | Mtu anaestahiki kuweka Stempu Hati ya awali. |
| 19. | Hati ya ukodishaji meli au sehemu ya meli | 0.5% | anayekodisha |
| 20. | Hundi, kwa kila hundi moja | 500/= | Mpokeaji wa hundi |
| 21. | Ushuru wa Mtaji<br>(a) Mtaji wa hisa inayojulikana ongezeko lake kwa Kampuni yoyote iliyoanzishwa Zanzibar na kuweka jukumu maalum – jumla ya thamani.<br>(b) Mtaji wa hisa ulioongezwa kwa kampuni ikiwa ongezeko hilo ni sharti la kutoa mkopo kwa kuendeleza mradi<br>(c) Ikiwa imetangazwa kupitia ubadilishaji wa hisa | <br>0.5%<br><br>Hapana<br><br>Hapana | Muhusika |
| 22. | Nakala au sehemu | 5,000/= | Mtu ambae nakla imefanywa kwa niaba yake |
| 23. | Nakala au kivuli cha Hati kinachotozwa ushuru ambacho ushuru wa mali hiyo umelipwa | 5,000/= | Anaestahiki kulipa kwa hati ya awali. |
| 24. | Nakla ya ukodishaji | 5,000/= | Mkodishaji |
| 25. | Hati ya Ubunifu (Hati ya uhaulishaji wa mali kwa mdai kwa maslahi ya wadaiwa wake) ya jumla ya thamani | 0.5% | Mdaiwa. |

| Nam. | AINA YA HATI | USHURU WA STEMPU | MTU ANAEPASWA KULIPA |
|---|---|---|---|
| 26. | Mikataba inayohusiana na hisa | 0.1% | Mtekelezaji au wakala au kama hakuna utekelezaji au wakala mtu aliyetoa hati au taarifa |
| 27. | Uhaulishaji (ambao si uhamishaji wa mali) - kwa jumla ya thamani | 1% | Ataenunua au ataehaulishiwa. |
| 28. | Uhaulishaji, ikijumuisha uhaulishaji wa mali zilizowekewa rehani | 1% | Aliyesihiwa / aliyeekewa rehani |
| 29. | Dhamana za Forodha - jumla ya thamani | 0.05% | Mtu wa mwanzo aliyeitoa |
| 30. | Hati (Deed) | 5,000/= | Wahusika wa hati au mmoja yoyote kati ya hao. |
| 31. | Dhamana ya benki - ama dhamana ya rehani au vyenginevyo, ikiwa dhamana ya soko – ya jumla ya thamani. | 0.5% isizidi 100,000/= | Anaeitoa. |
| 32. | Dhamana ya benki au hisa | 1% | Anaeitoa. |
| 33. | Hati ya usitishwaji wa Ubia | 10,000/= | Anaeitoa. |
| 34. | Talaka - (hati yoyote inayoondoa uwepo wa ndoa) | 5,000/= | Mtoaji . |
| 35. | Rehani inayohusiana na ardhi iliyozingatia usawa - jumla ya thamani. | 0.5% | Mueka rehani |
| 36. | Ubadilishaji wa mali - jumla ya thamani. | 0.5% | Anaebadilisha |
| 37. | Nakala (Extracts) | 5,000/= | Anaeitoa |
| 38. | Malipo ya ziada - hati yoyote inayotozwa malipo ya ziada kwa rehani inayohusiana na ardhi. | 0.5% | mdhaminiwa |

| Nam. | AINA YA HATI | USHURU WA STEMPU | MTU ANAEPASWA KULIPA |
|---|---|---|---|
| 39. | Hiba – hati isiyokuwa na malipo zaidi katika rehani za mali- ya jumla ya thamani. | 1% | anayeitoa |
| 40. | Makubaliano ya kukodishwa kwa madhumuni ya kununua - ya jumla ya thamani. | 1% | Anayenunua |
| 41. | Hati ya kizuizi au pingamizi | 10,000/= | Anayeweka pingamizi |
| 42. | Hati ya Dhamana ya Ushuru. | 1% | Mtoaji wa hati |
| 43. | Dhamana ya utekelezaji wa Bima | 20,000/= | Anayetoa dhamana |
| 44. | Bima ya Maisha. | 0.5% | Kampuni au mtu anaetoa Bima. |
| 45. | Kodi ya Ardhi — jumla ya thamani. | 1% | Mkodishwaji. |
| | Kodi nyenginezo | 0.5% | Mkodishaji |
| 46. | Barua ya mkopo – hati ambayo mtu mmoja anamuidhinisha mtu mwengine kutoa mkopo kwa mtu kwa niaba yake. | 5,000/= | anayekopeshwa |
| 47. | Barua ya leseni – makubaliano yoyote kati ya mdai na mdaiwa wake ambayo barua itakuwa na muda maalum utaakhirisha deni na kumruhusu mdaiwa kuendelea na biashara kwa mujibu wa maamuzi yake. | 5,000/= | mdaiwa |
| 48. | Mkopo | 0.5% Isiyozidi 100,000/= | anaehitaji |
| 49. | Bima ya Baharini – thamani ya | 0.5% | Kampuni au mtu anaetoa Bima. |

| Nam. | AINA YA HATI | USHURU WA STEMPU | MTU ANAEPASWA KULIPA |
|---|---|---|---|
| 50. | Makubaliano ya kuanzisha Kampuni | 20,000/= | Kampuni. |
| 51. | (a) Hati ya rehani-thamani ya rehani ambayo inatoa uwakala kisheria kukusanya kodi ya mali iliwekwa rehani ambayo inatoa umiliki kwa maana ya kipengele hiki. | 0.1% | Mtu anaeitoa |
| | (b) Endapo dhamana ya jumla au ya ziada au iliyofuatia imetolewa kwa njia ya dhamana nyengine ambapo dhamana ya awali imewekwa stempu sahihi. | 5,000/= | Mtu anaeitoa |
| 52. | Kitendo cha kuapisha-kilichofanywa muapishaji katika kutekeleza wajibu wa ofisi yake, au mtu mwengine yoyote mwenye mamlaka ya kisheria kama muapishaji. | 5,000/= | Mtu anaehitaji kiapo. |
| 53. | Hati ya mgawanyo | 0.5% | Wahusika kwa mujibu wa hisa zao ya mali yote inayogaiwa. |
| 54. | Hati ya Ubia. | 20,000/= | Wabia wote |
| 55. | Sera za Bima | 20,000/= | Kampuni au mtu anaeitoa sera au anayemiliki sera ya bima |
| 56. | Hati ya Kukataza au hawala-maelezo yoyote ya maandishi yanayofanywa na Muapishaji, anayeapa kukataa hati ya malipo na hawala ya fedha. | 5,000/= | Mtekelezaji wa hati |
| 57. | Hati ya Uwakala. | 5,000/= | Mtekelezaji wa hati |

| Nam. | AINA YA HATI | USHURU WA STEMPU | MTU ANAEPASWA KULIPA |
|---|---|---|---|
| 58. | Risiti au Hati ya mauzo kwa makubaliano ya mkataba wa mapatano chini ya sheria hii. | Shilingi 30 kwa kila Shilingi 1000 (3%) mauzo ya jumla, jumla ya risiti za malipo (kwa ajili ya mauzo ya bidhaa au huduma). | Mtoa risiti |
| 59. | Uhaulishaji mpya wa rehani ya mali - jumla ya thamani. | 0.01/= | Anayewekewa rehani |
| 60. | Ruhusa- hati yoyote ambayo si ruhusa iliyoelezwa na ambayo mtu ametangaza malalamiko juu yake kwa mtu mwengine au kwa mali iliyoelezwa. | 5,000/= | anayepatiwa ruhusa |
| 61. | Usawazishaji: hati yoyote (inajumuisha hati ya muombaji au anayekataa) | 0.5% | Mtu anayeomba usuluhishi au usawazishaji |
| 62. | Hati ya usafirishaji kwa njia ya meli - kwa au kuhusiana na uhaulishaji wa bidhaa kwa upakizi katika chombo cha Bahari. | 5,000 /= | Mtu anayetoa amri ya usafirishaji |
| 63. | Tamko la kisheria | 5,000/= | Mtu anaetoa Tamko |
| 64. | Kutoa hati ya ukodishaji | 5,000/= | Anayetoa hati |
| 65. | Uhaulishaji.<br><br>(a) Thamani ya jumla ya Hisa. | 1% | anayehaulishiwa |
| | (b) wa hisa katika kampuni zilizoorodheshwa katika masoko ya hisa inayotokana na biashara ya hisa hizo katika masoko ya hisa. | 0.5% | anayehaulishiwa |
| | (c) wa mali kwa madhumuni maalum ya kuiweka mali kwa kuiweka tena katika dhamana chombo | Hapana | |

| Nam. | AINA YA HATI | USHURU WA STEMPU | MTU ANAEPASWA KULIPA |
|---|---|---|---|
| 66. | Dhamana – kuhusiana na mali iliyofanywa kwa maandishi yoyote isiyokuwa wasia. | 5,000 /= | Anayepatiwa dhamana |
| 67. | Uhaulishaji wa Hisa au dhamna za hisa - kwa mmiliki iliyotolewa chini ya Sheria ya Kampuni – ya thamani ya jumla. | 1% | Mmiliki wa Hisa |
| 68. | Uhaulishaji wa hisa | 0.1% | Mnunuzi au anayehaulishiwa |

## JADWELI LA PILI

### MFUMO WA MALIPO YA MKUPUO
### (CHINI YA KIFUNGU CHA 60)

| | Mauzo kwa TZS | Kiwango 'TZS' kwa mwaka |
|---|---|---|
| 1. | Ikiwa mauzo yasiyozidi Shilingi za Tanzania 2,000,000 | Hapana |
| 2. | Ikiwa mauzo yanayozidi Shilingi za Tanzania 2,000,000 lakini yasiyozidi 3,500,000 | 200,000 |
| 3. | Ikiwa mauzo yanayozidi Shilingi za Tanzania 3,500,000 lakini yasiyozidi 5,000,000 | TZS. 200,000 +3.5% ya ziada ya TZS. 3,500,000 |
| 4. | Ikiwa mauzo yanayozidi Shilingi za Tanzania 5,000,000 lakini yasiyozidi 7,000,000 | TZS. 252,500 +4% ya ziada ya TZS. 5,000,000 |
| 5. | Ikiwa mauzo yanayozidi Shilingi za Tanzania 7,000,000 lakini yasiyozidi 10,000,000 | TZS. 332,500 + 4.5% ya ziada TZS. 7,000,000 |
| 6. | Ikiwa mauzo yanayozidi Shilingi za Tanzania 10,000,000 lakini yasiyozidi 12,000,000 | TZS. 467,500 + 5.0 % ya ziada ya 10,000,000 |
| 7. | Ikiwa mauzo yanayozidi Shilingi za Tanzania 12,000,000 lakini yasiyozidi 15,000,000 | TZS. 567,500+ 5.5 % ya ziada ya TZS. 12,000,000 |

**JADWELI LA TATU**

**Watoa huduma za Usafiri**

**(Chini ya kifungu cha 3)**

---

| | Huduma za usafiri | Maelezo | Ushuru wa Stempu |
|---|---|---|---|
| 1. | Gari za Abiria /Skuli na Wafanyakazi | | 400,000 |
| 2. | Vyombo vya maringi matatu | | 200,000 |
| 3. | Gari za kukodisha (abiria 1-6) | | 500,000 |
| 4. | Gari za kukodisha (zaidi ya abiria -6) | | 700,000 |
| 5. | Vyombo vya moto | Abiria 8-14 | 250,000 |
| | | Abiria 15-24 | 500,000 |
| | | Abiria 25-36 | 600,000 |
| | | Abiria 37 na zaidi | 700,000 |
| 6. | Taxi Wote | | 400,000 |
| 7. | Skuli za Udereva | | 400,000 |
| 8. | Gari za Mizigo | Zaidi ya Tani 10 | 1,000,000 |
| | | Tani 8 isiyozidi tani 9 | 700,000 |
| | | Tani 4 hadi tani 7 | 500,000 |
| | | Tani 1 hadi tani 3 | 300,000 |
| | | Tani 10 au chini yake ikiwa imeungana na kibebea mizigo kinachozi tani 15 lakini kisichozidi tani 20. | 1,200,000 |

## JADWELI LA NNE

**(Chini ya kifungu cha 60 (1) (b))**

---

## USHURU WA STEMPU KWA KILA MWEZI

| Nam. | Mauzo ya mwaka | Asilimia |
|---|---|---|
| 1. | Mauzo ya mwaka yanayozidi Milioni 15 hadi Milioni 29 | asilimia 3% ya jumla ya mauzo |
| 2. | Bidhaa na huduma zinazoingizwa nchini ambazo zimesamehewa Kodi ya Ongezeko la Thamani | 2% ya jumla ya mauzo |

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 21 Juni, 2017.

.................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)
***Katibu wa Baraza la Wawakilishi***
***Zanzibar***